

## **ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

### **MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

- |                                       |   |
|---------------------------------------|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali               | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.   |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa        | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.  |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma             | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.   |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi          | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.              |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.                   |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee              | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.   |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri               | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji       | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.                    |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed       | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.                      |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary        | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.  |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman         | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.  |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban      | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.                           |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji                | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.                                 |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed          | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.    |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan         | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.  |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna            | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.                                     |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya          | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.  |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui           | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.                                   |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk              | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.                           |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman           | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.            |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali              | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.                                  |
| 22.Mhe. Machano Othman Said           | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.                                     |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan       | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.   |

24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi/Jimbo la Mpandae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

**Ndugu Yahya Khamis Hamad**

**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Sita - Tarehe 28 Januari, 2015**

*(Kikao kilianza Saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti, (Mahamoud Muhammed Mussa) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Boara:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya uwasilishaji Mswada wa Sheria ya Maandili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo mengine Yanayohusiana na hayo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa shughuli za kujadili Mswada huu katika Kamati zilichukua muda mrefu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe kwanza wasilisha hati Mezani.

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa).** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani taarifa ya Kamati ya Viongozi Wakuu wa Serikali kuhusiana na Mswada wa Maadili ya Viongozi wa Siasa.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 24**

**Watuhumiwa wa Jinai Kupelekwa Nje ya Nchi.**

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Salim Abdalla Hamad) – Aliuliza:-**

Hivi karibuni baadhi ya wananchi wamekamatwa kutokana na sababu wanazozielewa wakamataji na kupelekwa Tanzania Bara kwa kufunguliwa kesi katika Mahakama ya Tanzania Bara.

- (a) Kwa nini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikaridhia utaratibu huo wakati Zanzibar ni nchi na yenye Mahakama zenye hadhi mbali mbali.
- (b) Ni sheria gani iliyotumika na kwa makosa ya aina gani inayohusu Mzanzibari mtuhumiwa kukamatwa Zanzibar na kupelekwa Tanzania Bara kufunguliwa kesi huko huko Tanzania Bara.
- (c) Serikali inatoa tamko gani kuhusu mazingira haya ambayo Wazanzibari wengi anawatia hofu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 24 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- a) Mhe.Mwenyekiti, utaratibu wa kisheria katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola ni kwamba nchi yenye Mamlaka ya kumfikisha muhalifu Mahakamani na kumshitaki ni ile ambayo ndani ya nchi hiyo tukio husika la kihalifu limetokea. Hivyo, endapo tukio la kihalifu limetokea Tanzania Bara, watuhumiwa wanaweza kushitakiwa Tanzania Bara na endapo uhalifu umetokea Zanzibar, Mahakama za Zanzibar zinaweza pia kuwashitaki watuhumiwa hao.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo, Katiba ya Zanzibar ya 1984, kifungu cha 101, kinaweka masharti ya kikatiba ya utaratibu wa utekekelezaji wa Hati za Mahakama katika Zanzibar na Tanzania Bara kwa ujumla. Na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 124 imeweka masharti kama yale yaliyomo kwenye kifungu cha 101 cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo na kwa mujibu wa masharti ya vifungu vyta Katiba nilivyovitaja ni utaratibu halali wa kisheria wa mtu kukamatwa upande mmoja wa Muungano na kupelekwa upande mwengine wa Muungano endapo uhalifu huo umetokea na kutendwa katika eneo (*Jurisdiction*) husika.

- (b) Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza misingi ya Katiba zetu mbili zilivyo, kuna utaratibu pia wa kisheria ambapo Mzanzibari au Mtanzania ye yote ambae atatuhumiwa kutenda kosa lolote la uhalifu Nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anaweza kukamatwa na kupelekwa nchi ambayo anatuhumiwa kutenda kosa na kushitakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hizo ni sheria ya kubadilishana Wahalifu, Sura ya 368 (*Extradition Act Cap. 368*) na Sheria ya Kuysaidiana katika mambo ya Jinai Sura ya 254 (*The Mutual Assistance in Criminal matters Act, Cap. 254*). Sheria hizo zinaweka masharti na utaratibu wa kubadilishana Wahalifu.

- (c) Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaongozwa kwa misingi ya Sheria na Katiba hivyo wote tuna wajibu kuhestimu Katiba na Sheria zilizopo na endapo mtu anatuhumiwa kutenda kosa, basi Sheria zitatumika bila ya kumuonea au kumkandamiza mtu ye yote.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa wananchi na taasisi zote za Serikali tuongozwe na misingi ya Sheria na tujiepushe na uvunjifu wa sheria.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza suali moja la nyongeza lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Kwa kuwa tulidhani kuwa lile tokeo la Darajani ndilo watuhumiwa hawa liliwafanya wakamatwe na sitokeo lililotokea Bara ni tokeo hili lililotokea hapa Zanzibar wale maustadh siku ile kutoke bomu pale, baada ya muda mfupi na wao wakamatwa kama watuhumiwa. Na kwa kuwa Zanzibar ina uzoefu wa kuendesha kesi kubwa kubwa za uhaini kama tulivyoendesha ile kesi ya mauaji ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, chini ya uongozi wa jaji Mkuu Ali Haji Pandu na Mwanasheria Mkuu Dorado.

- a) Ni sababu gani za msingi zilizopelekea Mheshimiwa hawa Mashehe wetu kukamatwa wakapelekwa Bara kudhalilishwa na kufanyiwa vitendo viovu vyta kiharamia.
- b) Kwa kuwa asilimia kubwa ya Wazanzibari ni waislam na kwa kuwa wanaonyanyaswa na kudhalilishwa kule ni waislam wenzao na kwa mujibu wa taarifa tulizonazo wengine wanafanyiwa matendo ya kiharamia kama kudhalilishwa kijinsia, Je, Waislam waliobaki hapa wakija kuamua kufuata maelekezo ya dini yao kwamba *Almuslim Mansalama Muslimina min lisanih wayadihi*. Wakija wakifuata maelekezo ya dini yao wakiamua kuyatetea si nyie Serikali mtakuwa mmesababisha vurumai hilo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe kwa mujibu wa Kanuni ya 40, kifungu kidogo cha 3, swala moja la msingi lina masuala ya nyongeza (a) na (b) sio (c).

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Haya basi jibu hayo niliyokwishapata.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Jibu langu la msingi nimeeleza bayana kabisa kwamba unapotuhumiwa kutenda kosa, pale ambapo umetenda kosa ikiwa ni Tanzania Bara ama Zanzibar ndipo

unaposhitakiwa, ndugu zetu walioshitakiwa wenyewe kesi Mahakamani sasa, hawakushitakiwa kwa mujibu wa maelezo kwa tukio lililotokea Darajani, kwa maelezo ya huko kwenye utaratibu wa kesi ni kwamba makosa hayo yametokea upande wa Tanzania Bara ndio maana kesi hiyo inaendelea upande wa Tanzania Bara.

Sasa ni haki ya watuhumiwa kuthibitisha Mahakamani kwamba wao hawakutenda kosa na kwa vyovypote vile unavyotoa ushahidi kwa ukamilisho katika Mahakama, Mahakama kwa njia moja au nyengine ndiyo inayopaswa kuamua nini kinachoendelea, hakuna mwanadamu yejote anayempendelea mwanadamu mwenzake adhalilike, apate matatizo ama aweko ndani, hususan Serikali na wananchi wote hawapendi kabisa kumuona mwengine anadhalilika, lakini utaratibu wa kisheria tuliojiwekea katika nchi ndio ambao unatuwekea mipaka ya kufuata zile taratibu, cha msingi hapa ni wale watuhumiwa kuthibitisha Mahakamani wanakosa ama hawana kosa, kesi inaendelea huko Tanzania Bara.

Kwa vyovypote vile kwa sababu kesi iko Mahakamani na kwa mujibu wa Kanuni zetu na taratibu zetu hatupaswi sana kuzungumzia yanayoendelea Mahakamani. Hivyo, niwaombe watuhumiwa kwa kupitia mawakili wao kueleza vizuri katika ushahidi wao na hairuhusiwi kumdhaililisha mtu aliyeo ndani kwa namna yoyote ile. Kwa hivyo, vile vili, kama kuna lolote la jambo hilo washtakiwa wana haki ya kisheria kueleza mambo hayo kupitia kwa wenywewe ama kwa wakili wao, ili kuihakikishia Mahakama na vitendo hivyo ni kinyume na utaratibu.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi na mimi kuuliza suala moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja.

- a) Kwa kuwa Mahakama ipo Zanzibar, je, watuhumiwa wanaokamatwa Tanzania Bara wanaweza kushitakiwa Zanzibar.
- b) Nani na watuhumiwa gani waliothumiwa na kushitakiwa Zanzibar kutoka Tanzania Bara na kosa gani kubwa ambalo wamefanya watuhumiwa hao Mahakama ya Zanzibar na ikaweza kushindwa kuwashukumu wahukumiwa hao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Suala la msingi nilieleza hivyo hivyo ambavyo Mheshimiwa Mwanajuma, ameuliza, naomba nirudie kulisema ili yeze aweze kuelewa na wananchi wengine waelewe.

Kwamba ni utaratibu wa kisheria katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola, ni kwamba nchi yenyewe mamlaka ya kumfikisha muhalifu Mahakamani na kumshitaki ni ile ambayo ndani ya nchi hiyo tukio husika la kihalifu limetokea, hivyo endapo tukio la kihalifu limetokea Tanzania Bara watuhumiwa wanaweza kushtakiwa Tanzania Bara na endapo uhalifu umetokea Tanzania Zanzibar, basi Mahakama ya Zanzibar inaweza kuwashitaki watuhumiwa hao.

Kwa hivyo, inategemea pale ambapo tukio limetokea ndipo pale ambapo mtu anashitakiwa, kwa hivyo, wapo ambao wametenda makosa hapa na wakakimbilia Tanzania Bara na wakakamatwa, wakaletwa Zanzibar na kushtakiwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa sasa siwezi kukumbuka majina ya watu hao, lakini ni utaratibu wa kawaida, kila mmoja hili analielewaa, kwa hivyo, ninachosema hapa kwamba cha msingi ni kufuata taratibu za kisheria na pale mtu anapoona taratibu zimevunjwa, zipo taratibu vile vili za kufuata kupitia Mahakama ili kuonyesha kwamba utaratibu fulani umevunjwa ili Sheria ichukue mkondo wake.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri, swala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa kuna uvumi kwamba washitakiwa wale wanatendewa vitendo visivyo vya kibinaadamu, yaani vitendo vya kudhalilishwa na kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na haki za binadamu na kwa kuwa Serikali yetu ya Zanzibar moja katika *commitment* yake ni kuhakikisha kwamba raia zake hawafanyiwi vitendo ambavyo ni kinyume na haki za binaadam.

- (a) Je, Serikali imechukua hatua gani kufanya utafiti kama huo uvumi unaosemwa ni kweli au laa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Serikali ni wajibu wake kuhakikisha kwamba wananchi wake wote hawafanyiwi vitendo vya kudhalilishwa na ni haki na wajibu wa Serikali kufuatilia jambo hilo, kwa mpaka sasa Serikali ilipofuatilia haijapata uthibitisho wa kuona matendo hayo yamefanyika.

Hata hivyo, tutazidi kuendelea na uchunguzi tutatute zaidi na zaidi ili kuthibitisha tuhuma hizo ambazo ni uvumi ambaa haupaswi kutokea hasa kwa watendaji walinzi wa nchi, ama walinzi wa wafungwa kutokea kufanyika vitendo vyovoyote vile vya udhalilishaji, ni kosa ni kinyume na utaratibu ni kinyume na sheria.

## Nam. 2

### Njia Mbadala ya Kupunguza Hewa Ukaa.

**Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-**

Katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa mvua nchini lililosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Ngoyay Lowasa, aliwahi kuja na mpango wa kuzalisha mvua kwa njia ya kemia (*chemical synthetic rain*), mpango ambaa haukufanikiwa kutokana na ukubwa wa gharama zake.

Na kwa kuwa kupitia mabadiliko hayo hayo ya tabia ya nchi kumekuwa na ongezeko kubwa la hewa ukaa ( $CO_2$ ) katika mazingira tunayoishi, ambayo siyo tu inaathiri mazingira yetu pekee, lakini inaweza kuathiri hata afya za viumbe mbali mbali wanaoishi katika mazingira hayo na kuharibu mfumo mzima wa kuimarisha mazingira husika.

Je, ukiachilia ile njia ya kupanda miti, pamoja na kutunza mazingira, hakuna njia nyengine mbadala na ya haraka kuweza kupunguza hewa ukaa katika mazingira yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: - Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi, swali lake nambari 2 lenye kifungu (a) na (b). kwanza naomba nitoe maelezo ya kina kwanza kuhusiana na suala hili la kitaalam kama ifuatavyo:-

Chanzo kikubwa cha mabadiliko ya tabianchi ni kuonegezeka kwa joto duniani kunakosababishwa na kuongezeka kwa hewa chafu kwenye usawa wa dunia, mfano wa hewa chafu au gesi joto hizo ni kama hewa ukaa, yaani *carbon dioxide, methene, nitrous oxide, perfluorocarbons, hydrochlorocarbons, sulfur hexafluoride* na aina ya hewa hizo.

Hewa ukaa yaani *carbon dioxide* inachangia kwa asilimia 70 kwenye suala zima la mabadiliko ya tabianchi duniani, hewa hizo chafu zimeongezeka kwa kiwango kikubwa kuliko kiwango halisi kinachohitajika kuwezesha uhai na mifumo ya ki-solojia kuwa katika hali yake ya asili. Ongezeko la hewa chafu linazosababishwa mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na hewa ukaa linatokana na shughuli za kila siku za mwanadamu za viwanda, usafiri na usafirishaji, ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu.

Mhe. Mwenyekiti, nchi za Afrika zinachangia kiwango kidogo cha uzalishaji wa hewa chafu yaani *carbon dioxide*, Tanzania nayo inahisabika kuwa ni mionganoni mwa nchi zinazozalisha chini ya asilimia moja ya hewa ukaa tofauti

na kiwango ambacho kinazalishwa na Mataifa mbali mbali duniani ikiwemo Marekani, India, Brazil na aina ya nchi hizo zilizoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya kina sasa naomba kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi, suala lake kwamba hakuna njia nyengine mbadala na ya haraka ya kuweza kupunguza hewa ukaa katika mazingira yetu zaidi ya ile ya kupanda miti na kuhifadhi mazingira yetu.

|Mhe. Mwenyekiti, jitihada za upandaji wa miti kwa wingi zinazofanywa na nchi masikini ikiwemo Zanzibar ni kuwezesha unyonyaji ya hewa ukaa inayozalisha sehemu mbali mbali. Kuacha kupanda miti na kuruhusu kuendelea na ukubwa wa tatizo ambalo sisi ndio waathirika wakumbwa na zaidi kwamba uwezo wetu wa kuhimili athari zinazojitekeza ni mdogo katika nyanja zote za kifedha, kielimu na kiteknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwaomba wananchi wote wa Zanzibar kuendelea na juhudzi za kupanda miti kwa wingi hasa ile ya matunda na tuepuke tabia ya ukataji miti ovyo na uharibu wa misitu ili kusaidia katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba niulize swalii dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba hakuna njia mbadala ya kupunguza hewa ukaa zaidi ya kupanda miti na kuhamisiana kupanda miti na kwa kuwa ni jana tu tumeshapitisha sheria hapa ya kukuza na kuhifadhi mazingira, kwa hivyo, mazingira sasa itakuwa ina sheria itakayowalinda na kwa kuwa wananchi wanahamasika katika suala zima la kutunza mazingira kwa kuwanzisha vikundi mbali mbali vyta kuweza kupanda miti viwe vyta mazingira, vikiwemo vyta kupanda miti kama vile *VECA* iliyokuwepo kule katika jimbo langu, Vitongoji *Environmental Conservation* ambayo iko Vitongoji.

- a) Je, serikali mna mpango gani wa kuweza kuhamasisha na kutoa motisha kwa wananchi. Kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara huwa wanatoa zawadi kwa washindi wa kupanda miti. Je, nyinyi SMZ mna mpango gani wa kuweka *moral* kwa hizi jumuiya pamoja na vikundi mbali mbali vyta akina mama vilivyojiwekeza katika suala zima la upandaji miti ili wakawenza kupata moyo zaidi wa kupanda hiyo miti.
- b) Kwa kuwa Mheshimiwa aliyekuwa Edward Ngoyaye Lowasa, alishindwa kuleta ile mvua ya kutengeneza yaani *synthetic rain*, ule mpango wake ulifeli kwa *geographer* kubwa ya nchi yake na kwa kuwa hapa Zanzibar nchi yetu ni ndogo, mna mpango gani wa Serikali wa kuweza kulifuata lile wazo la aliyekuwa Waziri Mkuu wa Nchi hii, yaani Edward Ngoyaye Lowasa, kwa kuweza kutengeneza mvua, yaani *synthetic rain*, ili kuweza kupunguza makali ya mabadiliko ya tabianchi na mvua kwa sababu tupo katika kilimo. Je, mpango huo mnawenza mkaanzisha wa kutengeneza mvua.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tunashukuru sana kwamba wananchi wengi wana muamko kwa kipindi sasa cha kujaribu kutunza mazingira na kufanya shughuli za kuwa na vikundi vyta upandaji miti. Kwa taarifa ya Mheshimiwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni kwamba serikali kinaelewa na kwa kweli kuanzishwa kwa vikundi hivyo ni jitihada za serikali kuititia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Idara ya Misitu kuititia Idara ya Kilimo, kwa pamoja tunahamasisha na tunawapa motisha baadhi ya vikundi hivyo na tayari tumeweza kuwasaidia.

Lakini kwa kuwa uwezo ni mdogo hatujaweza kuvifikia vyote kwa pamoja. Lakini tunavifahamu, tunavitembelea na kuwapa moyo na kujaribu kutatua matatizo ambayo wanakabiliana nayo, hasa katika masuala ya kitaalamu katika kuona kwamba jitihada hizo za wananchi zinathaminiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba nchi ya Zanzibar kuweza kutengeneza mvua ambayo anaiita *synthetic rain*, naomba Mhe. Mwenyekiti, hili tulichukue ni suala la kitaalamu, linahitaji utafiti, basi kama serikali ikiweza kufanya utafiti na kuona linawezekana bila ya athari zozote, bila ya shaka itaweza kuwezekana. Kwa sababu hivi ni suala ambalo linahitaji utafiri. Nasema tunalichukua kwa kushauriana na wataalamu wetu na kuona kwamba linaweza kutekelezwa kama kule Tanzania Bara limeweza kushindikana.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kumuuliza Mhe. Waziri katika Ofisi ya Kwanza wa Rais swali la nyongeza lenye kifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:

- a) Mhe. Waziri, anaweza kutueleza kitaalamu uhusiano wa hewa mkaa na upandaji wa miti kwa maana kwamba kuwa na miti mingi yenye rangi ya kijani, yaani uhusiano wa kitaalamu.
- b) Mhe. Mwenyekiti, upandaji wa miti au uhifadhi wa misitu ni moja katika hatua za matumizi ya hewa mkaa. Namuuliza Mhe. Waziri, ni vikundi vingapi na ni vipi viliviyopata msaada kutoka shirika lolote lile la kimataifa kwa sababu tu wamefanya juhudu ama ya kuhifadhi misitu au ya kupanga miti.
- c) Kama kuwa na miti mingi...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, naomba ujibu maswali yake mawili, hilo la tatu silo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu tunapojobu maswali wawe wanasikiliza yale majibu, kwa sababu hichi anachikiuliza ni cha kitaalamu kweli na nimeshakieleza katika kujibu swali langu.

- a) Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa faida zaidi, naomba nimuarifu kwamba uhusiano uliopo kati ya kupanda miti na kupunguza hewa ukaa yaani *carbon dioxide*, nikikumbuka sayansi yangu ya darasa la siti kwamba, miti inahitaji kuinyonya *carbon dioxide* iliyopo kwenye hewa kwa ajili ya kutengeneza chakula chake. Kwa hiyo, tunahitaji *process* inayoitwa *photothynthesis*. Kwa hiyo, upandaji wa miti kwa wingi ni kuweza kuinyonya ile hewa ambayo ni chafu na kuweza kupunguza uharibu wa mazingira ndani ya visiwa vyetu na ndani ya dunia. Huo ndio uhusiano amba mimi naufahamu, lakini kama upo zaidi.
- b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili ni suala ambalo linahitaji takwimu kwa sababu vikundi ni vingi na shughuli hii inafanywa kwa pamoja kati ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuititia Idara ya Mazingira, lakini pia, kuititia Idara ya Misitu na Wizara ya Kilimo. Naomba jibu hili tumletee kwa maandishi. Ni kweli kuna vikundi vingi, lakini kuna misaada mbali mbali kutoka jumuia ambazo zio za kiserikali na kutokana leo katika mataifa mbali mbali ambayo yamesaidia jitihada hizi. Naomba jibu hili tumletee kwa maandishi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa anajibu swali la msingi aliasia miti kutokukatwa. Mimi nataka kujua hizi bekari zinatumia gezi au hakuna mtu asiokula mkate wa boflo kati siye na wananchi au ndio ule msemo wetu tunaosema "nguruwe haramu mchuzi wake unakunywa". Leo maisha ya shamba kukata fito mbili hasa Kijiji cha Pete jimbo la Muyuni, kuna baadhi ya watu tena wanafunzi hutiwa ndani. Mimi nataka kujua bekari zinatumia gesi au hizi kuni zinatoka wapi. Ikiwa mwananchi wa jimbo la Muyuni kakata fito mbili tu tena ni mwanafunzi anahukumiwa kwenda ndani.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali moja la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kama ifuatavyo. Ni vizuri kwamba amelileta, swali ni zuri sana.

Bekari zetu zote tulizonazo hapa ndani ya visiwa zinatumia kuni. Kuni maana yake kwamba tunakata miti. Kwa hivyo, serikali ipo katika jitihada za kuangalia jinsi gani zitaweza kutumia kuni chache au kutumia mfumo mwengine amba mchi yengine wameweza kutumia, mfano Kenya kwa kutumia *biogas* kwa ajili ya kutumia ndani ya mabekari yetu na majiko sanifu vile vile kwa ajili ya kupunguza matumizi makubwa ya kuni kwa maana ya kwamba miti inakatwa kwa wingi.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa kwamba bado wananchi wa Zanzibar hata mjini bado wapo wanatumia kama sio kuni lakini pia wanatumia mkaa maana yake ndio hapo kwamba miti inakatwa. Ni yote mawili tunahitaji, tunahitaji kuwa na miti iendelee, lakini pia, tunahitaji na maisha yaendelee kuwepo. Tunachowaomba sana Waheshimiwa wananchi wetu kwamba tuwe na tabia ya kwamba tunakata mti baada ya kupanda miti, hilo litatusaidia sana. Tunakata miti lakini wakati huo huo tuwe tunaipanda miti kwa wingi.

Lakini vile vile, serikali ipo katika jitihada za kuangalia na tayari kuna majaribio katika maeneo mengi ya kuweza kuwaka majiko sanifu, majiko ambayo yanatumia kuni chache sana au kuweza kutumia unga wa mbao katika matumizi ya kupika na kuweza kuzuia ukataji mkubwa wa miti. Lakini jitihada za kuwahamasisha wananchi ambao wanao uwezo wa kutumia gesi katika matumizi yao ya kila siku nazo zimo.

Lakini pia, serikali imo katika kutafakari jinsi gani kuweza kuwasaidia hasa wananchi wa vijijini waweze kuondokana na ukataji mkubwa wa miti kwa sababu wanahitaji kuishi wanahitaji kuwa na kuni katika maisha yao, lakini miti hiyo tunahitaji katika kutunza mazingira yetu na mazingira ndio maisha yenye, kwa hiyo, haya mambo yanategemeana.

#### Nam. 104

#### Mitihani Kuchapishwa kwa Watu Binafsi

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman** - Aliuliza:-

Serikali inastahili pongezi kwa kuweza kuiweka Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika hali nzuri ya ufanisi wa kazi zake za kila siku, pamoja na hali hiyo nzuri bado Idara hii haitumiki ipasavyo kwa kutopewa kazi nyeti za kuchapa kutoka serikalini.

- Naomba serikali itueleze ni kwanini Wizara ya Elimu haikuweza kupeleka kuchapisha Mitihani na badala yake kazi hiyo imepelekwa kwa watu binafasi.
- Je, kufanya hivyo si kunaipunguzia serikali mapato na kuwakosesha fedha walipa kodi wa nchi hii.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 104 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ina mashine za kisasa za kuchapishia kazi mbali mbali. Wizara yangu imetuwa na azma ya kuchapisha kazi zake mbali mbali katika kiwanda hicho. Kikawaida kutokana na unyeti wa kazi za mitihani Wizara huwa haibainishi mahali ambapo mitihani inachapishwa. Mitihani huwa inachapiswa kwa usiri mkubwa na kwa kuzingatia usalama na umakini wa mahali pauchapishaji. Upatikanaji wa vifaa mbali mbali vya kuchapishia na vifaa vyengine muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda kumjibu kama ifuatavyo:-

- Mhe. Mwenyekiti, napenda nikiri kuwa Wizara yangu haikuchapisha mitihani yake katika Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali licha ya juhudhi kubwa iliyoichukua kukutana na uongozi wa kiwanda hicho na kuandaa mipango ya pamoja kwa ajili ya kuchapisha mitihani hiyo. Katika mukutano wa pamoja ilionekana kuwa kiwanda hakikuwa na baadhi ya vifaa vya kuchapishia na kufungia mitihani kama vile karatasi mifuko. Uongozi wa kiwanda iliishauri Wizara inunue karatasi wenyewe kwa kuititia mzabuni waliomzoea na kiwanda kilitaka kilipwe kwa kazi za uchapishaji na ununuzi wa mifuko tu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudhi za haraka za Wizara kufanya zabuni ya manunuvi ya karatasi, uongozi wa kiwanda hawakuridhika na mzabuni alieshinda na kuwa tayari kuleta karatasi hizo. Kutokana na hilo, Wizara baada ya mashauriano iliamua kuchapisha Mitihani hiyo Tanzania Bara katika kiwanda kilicho na uzoefu wa kufanya kazi hizo na ilifanyika kwa wakati bila ya kuathiri ratiba ya mitihani.

Kiwanda hicho kiliweza kutoa huduma zote ikiwemo karatasi, mifuko ya kuingizia na kurejeshea mitihani. Aidha, kiwanda hicho kilipatiwa ulinzi kamili na serikali kuhakikisha kuwa kazi inafanyika kwa usalama wa hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, gharama zilizotumika katika kiwanda hicho ni za chini ulikinganisha na gharama za Mchapaji Mkoo wa Serikali. Gharama zote zilizotumika katika kampuni binafsi ziliwa ni Tshs. 275,185,578.79 ikijumuisha uchapishaji wa mifuko ya kuhifadhi na kurejeshea mitihani.

Kwa upande wa Kiwanda cha Mchapaji Mkoo wa Serikali gharama za uchapishaji ziliwa ni Tshs. 120,272,726/=, gharama za ununuzi wa karatasi za mzabuni waliompendekeza ziliwa ni Tshs. 159,300,000/= na gharama ya mifuko ya kutilia na kurejeshea mitihani ziliwa ni Tshs. 47,000,000/= na kufanya gharama zote kufikia Tshs. 326,572,726/=.

- (b) Mhe. Mwenyekiti, kuchapisha mitihani katika kiwanda binafsi haikuipunguzia serikali mapato bali Wizara imewenza kuokoa kiasi cha Tshs. 51,387,147.21 ambazo zimetumika kwa shughuli nyengine za ufanyaji wa mitihani kama vile ukodishaji wa usafiri na walini wa mitihani. Hata hivyo, Wizara yangu itaendelea na mazungumzo na Uongozi wa Kiwanda cha Mchapaji Mkoo wa Serikali kuhakikisha kuwa kwa siku za mbele kitawezza kuchapisha kazi zake katika kiwanda hicho.

**Mhe. Salma Mussa Bilali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri, una taarifa kwamba katika uchapishaji wa mitihani ya *Form II* kulikuwa na mchanganyiko baina ya somo moja na jengine. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri, je, suala hili ni kweli na kama ni kweli serikali imechukua hatua gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, naomba aniuilize tena kwa sababu sauti yake ipo chini sana hayupo karibu na *mic*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Jitahidi ili Mhe. Naibu Waziri, akusikie vizuri. Uliza tena swali lako.

**Mhe. Salma Mussa Bilali:** Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, kumekuwa na taarifa kwamba katika uchapishaji wa mitihani ya *Form II* kulikuwa kuna mchanganyiko baina ya mtihani mmoja na mwengine. Je, suala hili ni kweli na kama ni kweli serikali imechukua hatua gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri, naomba kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilali, swali lake la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, taarifa hizo si za kweli.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kabla ya kuuliza swali langu la nyongeza, naomba uniruhusu niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Elimu kwa uamuzi wake wa kuamua kujenga skuli ya ghorofa katika eneo la Muambe.

Mhe. Mwenyekiti, maamuzi hayo sio ya bure ni maamuzi halali kabisa kwa sababu kwa Pemba Skuli ya Muambe ni skuli pekee ambao wanafunzi wanaingia mikono mitatu na skuli pekee wanafunzi wanasoma dakika 20 kwa kipindi badala 40. Kwa hivyo, Serikali imetufanya haki na kwa kweli huo ndio uadilifu wenye.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri kama ifuatavyo:

Maamuzi ya kuchapisha mitihani hiyo Tanzania Bara ni maamuzi halali kwa sababu za msingi ambazo Serikali imetoa. Lakini, je, usalama wa mitihani hiyo ukoje. Lakini (b) hivi karibuni mmeteo matokeo ya mitihani kuna wengine wanasema hawakusikia yaktangazwa redioni hasa matokeo ya *Form II* na mmeteo kwenye mitandao. Huoni kwamba hatujafikia hatua hiyo kuwa Wazanzibari wengi hawajatumia huduma ya mtandao na kwa hivyo, hawajaweza kupata matokeo hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa, nilizungumza katika jibu langu mama kama mitihani hiyo ilichapishwa kwa usalama kwa sababu kulikuwa na ulinzi wa kutosha na ilitufikia mikononi ikiwa salama na ndio maana Mhe. Hija, hukusikia mara hii kama kuna mvujo, wanafunzi

wamejivisha *life jacket* kwa ajili ya mitihani ambayo inavuja, mitihani ilikwenda salama na hata katika matokeo ni wanafunzi wawili tu ambao tuliwagundua kufanya udanganyifu.

Suala la (b) ni kweli Mhe. Hija, kuwa matokeo mara hii tulitoa kwa njia ya mtandao hususan matokeo ya *Form II*. Na pili ni kweli nataka nikiri kama bado wanafunzi wetu hawajafikia *level* hiyo kubwa ya kuwa na *access* ya mitandao kwa sababu hata skuli zetu bado hazijawa zote takriban na *access* za mitandao. Lakini Mhe. Hija, kilichofanyika si tu kama tulitoa matokeo hayo kwenye mitando, lakini pia, tulitoa *hard copy* kwa ajili ya kubandika maskulini.

Na kwa mara ya kwanza Mheshimiwa, matokeo wanafunzi wameyapata baada ya siku mbili tu Wizara kutangaza kama sasa tuko tayari kutoa matokeo, kinyume na kipindi chote huwa tunatumia pesa nyngi ambazo Baraza la Mitihani hatuna, Idara ya Sekondari hatuna, tunatumia karibu 33,000,000 kila mwaka kwa ajili ya matangazo hayo kwa wiki moja, kama mnakumbuka Waheshimiwa.

Kwa hivyo, mara hii tuliamua kuzuia haya matumizi makubwa ambayo tunatumia na pesa ambayo hatuna kufanya njia nyepesi ya wanafunzi kupata matokeo yao mapema, lakini pia, kuweza kutumia vizuri hizi hizi pesa chache ambazo tunazo katika Idara zetu.

#### Nam. 57

#### **Uwekezaji katika Viwanda vya Minofu ya Samaki**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:-

Soko la samaki katika Ziwa Victoria limepanuka baada ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuwashawishi wawekezaji pamoja na kuwawekea mazingira mazuri ya biashara ya minofu ya samaki (*fish fillets*) na hivyo viwanda vingi vya kusindika minofu ya samaki kujengwa katika mji wa Mwanza. Kwa kuwa bahari ya Hindi inayo samaki wakubwa kama vile papa, nduaro, jodari na kadhalika ambao minofu yao ni mikubwa zaidi kuliko ile ya sangara.

Je, ni lini Serikali itawashawishi pamoja na kuwaakea mazingira mazuri kama yale yalioko Mwanza ili wawekezaji waje kuekeza hapa Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mwakilishi wa kudumu wa Jimbo la Wawi swali lake namba 57 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa uzalishaji wa samaki bado ni mdogo na unakidhi soko la ndani tu. Hivyo, Wizara yangu ilikuwa ikifanya juhudu mbali mbali za kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta ya uvuvi, ili kuongeza uzalishaji wa samaki ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda vya kusindika samaki. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya uvezeshaji na Taasisi nyengine, Wizara inawahamasisha wawekezaji na hivi sasa wawekezaji kadhaa ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika sekta ya uvuvi pamoja na kujenga viwanda vya samaki.

Ni matarajio yangu kuwa Wawekezaji hao wataweza kufanikisha kutimiza lengo hilo kutohana na mazingira ya uwekezaji yaliyoko hivi sasa Serikali.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa kila siku tunapata taarifa kwamba kuna wawekezaji wanakuja kuwekeza katika sehemu za samaki na kwa kuwa mara nyngi tunawaona wawekezaji wanaokuja ni wale wa sekta nyengine kwa mfano za utalii kiasi ambacho Zanzibar nzima imeja mahotelii.

- (a) Ni lini Serikali itazuia kabisa kuekeza katika mambo mengine haya na kuanza kutoa kipaumbele kwamba kuwataka wale wanaotaka kuwekeza katika mahotel sasa waje kwenye uvuvi kusudi asilimia 40 amba ni wavuvi wa nchi hii tuweze kupata soko la uhakika katika sekta hii ya uvuvi.
- (b) Kwa kuwa wenzetu katika ziwa Victoria kule wanafaidika mara tatu kutokana na ziwa lao lile, yaani wanapata samaki, wanaekea kwenye viwanda vya kusindika minofu, halkadhalika na mapanki ambayo ni mabaki yale yanayobakia baada ya kutoa minofu hutengenezewa mbolea. Sasa ikiwa wewekezaji hapana na juhudzi zimekwama, ni lini Serikali itachukua jukumu la kuweka viwanda vya kusindika yenye minofu kusudi tuweze kunufaika na sisi kwa kuweza kupata *three in one*, yaani kupata soko letu la samaki, pamoja na mambo kama ya viwanda vya kuweka vyakula vya kuku. Ni lini Serikali itaamua maamuzi hayo baada ya hawa wawekezaji kuwa wanakataa kataa sana kuwekeza katika sekta hii.

**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Ninakushukuru Mwenyekiti, Kwanza Sera ya Serikali ni biashara huria, haitawenza kabisa kuwazuia wawekezaji wa sekta nyengine, lakini vile vile, Serikali sasa hivi inafanya juhudzi kubwa ya kuwashawishi tena na wengine tayari wameshaanza kujitokeza kuweza kuwekeza kiwanda.

Lakini swali lako la pili, ni kweli kabisa niungane na wewe kuwa ziwa Victoria na jengine linahusiana na hayo yamepata mafanikio makubwa. Lakini kwa hapa kwetu Serikali bado haijafikiria kuweka viwanda vyake wenye we isipokuwa tutaenda katika *PPP (Private Partnership)* hivi karibuni na kiwanda hicho jana nilikuji katika suala lako kuwa Mhe. Rais alifanya ziara pale Comorom sasa tutakuwa na *full package* itakuja hapa ili kuweza kufanikisha katika azma ya kuweza kuwanuafaisha wavuvi wetu.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, ninakuru sana kunipa nafasi hii kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

- (a) Kwa kuwa Serikali ya Zanzibar ilikuwa na dhamira nzuri ya kuelekea uvuvi wa bahari kuu na mpaka sasa hivi hatujaona muelekeo wowote, Mhe. Waziri, dhamira hiyo nzuri imeshaondoka.
- (b) Kwa sababu wenzetu wa Mwanza wanafaidika na usindikaji wa samaki au minofu ya samaki na sisi bahari yetu tunayo nzuri na yenye samaki wengi, ili nasi tupate kusindika hiyo minofu ya samaki pamoja na mapanki aliyozungumza Mhe. Saleh. Ni lini wananchi wa Zanzibar watafaidika wakati kukiwa na viwanda pamoja na uzalishaji wa samaki kwa wingi kwa dhamira ya kuelekea uvuvi wa bahari kuu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, dhamira ya kwenda bahari kuu bado tunayo na tunaendeleza hilo, nadhani hivi karibuni tu utaweza kupata matokeo makubwa yatoendelea. Lakini bado nilikuwa nikianza kujibu jana na leo kuwa tuna muekezaji ambaye ameonesha nia kubwa na tayari *MOU* tunai-sign hivi karibuni kwa tayari amekuja na *full package*, tunaenda na bahari kuu kuweza kununua meli zile ambazo zitaweza kwenda bahari kuu.

Lakini na nyengine ni kuleta viwanda ambavyo tutaweza kusindika, lakini na jambo jengine kubwa la kufurahisha kwa hawa wavuvi wadogo wadogo wanaweza wakapatiwa boti, lakini hata yale mazao yao waje waweze kuuza katika kiwanda kile ili kuweza kufanikisha na kupata soko la uhakika.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi moja kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa, katika majibu yake mama Mhe. Naibu Waziri, alisema kwamba wawekezaji wataweza kufanikiwa kutimiza lengo hilo kutokana na mazingira mazuri ambayo Serikali imeyaweka. Swali langu kwamba ni mazingira gani mazuri yaliyowekwa na Serikali ya kuvutia wawekezaji hao ili waweze kuja kujenga viwanda hivyo vya kusindika samaki.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, mazingira mazuri kwanza ya Serikali yaliyowekwa ni kuwapa fursa nzuri wawekezaji wa nchi hii, lakini jengine miundombinu ambayo tayari mingi tumeanza kuiweka utakuwa shuhuda kuwa *airport* yetu tumeifungua vizuri, tuna miundombinu ya umeme iko vizuri na mengi mengineyo, hii ndio itakayokuwa fursa pekee kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika nchi yetu.

## Nam. 62

### **Mpango wa Kudhibiti Ongezeko la Bidhaa ya Samaki**

**Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-**

Kwa kuwa mahitaji ya matumizi ya samaki yanaongezeka na hasa kutokana na ongezeko la mahoteli ya kitalii kutumia bidhaa hiyo kwa wingi.

- (a) Je, Wizara ina mpango gani kukabili ana na tatizo hilo ili kutoa unafuu kwa wananchi kumudu bidhaa hiyo.
- (b) Je, Wizara haioni kwamba kutokuwa na mipango madhubuti kutapelekea kuingizwa kwa wingi samaki wasio na uhakika kwa afya za wananchi wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: - Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani swali lake nambari 62 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ina mipango madhubuti ya kuongeza upatikanaji wa samaki ili kukidhi mahitaji ya mahoteli ya kitalii na walaji.

Mikakati hiyo ni kuwezesha wavuvi kuvua katika kina kirefu cha maji ambapo hivi sasa Wizara yangu imeshawapatia mafunzo ya uvuvi wa bahari Kuu vijana 25 kutoka katika Chuo cha Uvuvi Mbegani, hatua hiyo kupelekea wengine zitaendelea kulingana na hali ya kifedha itakavyoruhusu.

Vile vile, mkakati mwengine ni kuwezesha uzalishaji wa samaki kwa njia ya ufugaji wa samaki na mazao ya mengine ya bahari yetu. Mikakati hii inaongezeka upatikanaji wa samaki nchini, hivyo itapunguza viwango vikubwa vyta ukosekaji wa samaki na utumiaji bora wa samaki katika nchi hii.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, wakati akijibu amesema kwamba Wizara imefanya jitihada za kutoa mafunzo kwa vijana 20.

- (a) Pamoja na mafunzo tatizo la nyenzo likoje kwa vijana waliopata mafunzo.
- (b) Kwa kuwa tayari kuna Kampuni binafsi za wazawa ambazo zimeonesha jitihada na zina uwezo wa kwenda kuvua samaki kwa kina kirefu ili kupunguza tatizo la walaji pamoja na kusaidia ajira kwa vijana. Mhe. Waziri, Wizara yake imejipanga vipi kutoa msaada kwa wale ambao wameanza kuonesha jitihada ya kutaka kuwekeza katika suala la uvuvi wa bahari kuu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimsawazishe tu sio vijana 20 ila ni vijana 25, lakini vile vile, huo ndio mwanzo tulioanza nao lakini na hali ikiruhusu basi tutawawezesha ili kufanikisha uvuvi huu.

Lakini swali lake la pili, Serikali iko tayari sasa kuwakaribisha wavuvi wote wa ndani au wawekezaji wote wa ndani na itatoa msaada mkubwa sana kila pale inapobidi.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika jitihada za Serikali kukabiliana na upungufu wa samaki nchini niliwashawishi wananchi kuanzisha mabwaya ya kufugia samaki na kwa kweli Mhe. Mwenyekitim wananchi walilopokea hilo na wakaanzisha mabwawa ya samaki na kwa kuwa wananchi wengi wamevunjika moyo kwa kukosa vifaranga nya samaki, je, ule mpango wa Serikali wa kuanzisha maabara ya kutoa vifaranga nya samaki kwa nini umekufa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwanza nia ya Serikali bado ni kuendeleza wafugaji wa samaki na hiyo unayoisema bado haijafa na hivi karibuni tu mwezi wa nne mwaka jana tulitiliana saini na washiriki wetu wa maendeleo *FAO* ili kuweza kujenga *hatcheries* mbili; moja ikiwa Pemba itajengwa katika Jimbo la Gando na moja Zanzibar katika sehemu ya Mkokotoni ili kuondoa basi ule upungufu wa vifaranga au tunasema *baby fish*.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kujua tu Mhe. Naibu Waziri, hawa vijana 25 mmepeleka Serikali ya Mapinduzi kwenda kusoma au ni msaada kutoka nje. Ukiachia hivyo, hivi sasa kumekuwa na kilio cha wakulima wa mwani kusaidiwa vifaa tu nya shilingi laki sita, laki saba, je, hasa Jimbo la Muyuni katika shehia ya Jambiani unatoa kauli gani kuhusu wakulima hawa kutokana kutokuwa na vifaa Wizara yako iko tayari kuwasaidia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Mwenyekiti, vijana 25 waliosomeshwa ni kuitia mradi wa bahari kuu, ni mradi wetu wenye ambao makao makuu yake yapo Fumba Mjini Zanzibar. Lakini Wizara yangu kwa hivi sasa haina bajeti ya kutosha, lakini pindi hali itakavyoruhusu itawasaidia wakulima hao.

#### Nam. 75

#### **Idadi ya Wastaifu waliopatiwa Kiunua Mgongo**

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad** - Aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi wa umma unapofika muda wao wa kustaifu hulazimika kustaifu. Na kwa kuwa watumishi hao kisheria hupata mafao yao ya kiinua mgongo na kubaki na shughuli nyengine za kujikimu kimaisha.

Je, kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 ni watumishi wangapi ambao wamepatiwa mafao yao ya kiinua mgongo.

**Mhe. Waziri wa Fedha** – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Bikame Yussfu Hamad, Mwakilishi wa Nafasi za Wanawake kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, malipo ya Kiinua Mgongo yanalipwa na Serikali Kuu kuitia Wizara ya Fedha na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*). Kwa wastaifu wanaolipwa na Wizara ya Fedha ni wale waliotumikia Serikali kabla ya kuanzishwa kwa mfuko wa *ZSSF* mwaka 1998. Kwa wastaifu wanaolipwa *ZSSF* ni wale waliojiunga na kuchangia katika mfuko wa *ZSSF* kuanzia mwaka 1998 hadi walipostaaifu.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2013/2014, Wizara ya Fedha imelipa jumla ya madai ya Kiinua Mgongo kwa wastaifu 872 kati ya wastaifu 1090 yenye thamani ya Tshs. 7.99 bilioni na madai ya Wastaifu 934 yenye thamani ya Tshs. 8.07 bilioni yamelipwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*).

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, aliyyoatoa lakini kuna malalamiko mengi ya wastaifu ambayo kuwa wengine wanafika miaka miwili, mitatu hawajapata kulipwa kiinua chao mgongo. Sasa kwa utaratibu wa utumishi wa umma kuna tarehe za kuajiriwa na kustaifu kwa ili kupatiwa hiyo fedha ya kiinua mgongo.

- a) Sasa, je, kwa nini utaratibu wa ulipaji unachukua muda mrefu kulipwa wastaafu hawa.
- b) Kwa sababu haya ni malalamiko ya wananchi, je, Mhe. Waziri, wizara yako ina kauli gani kupitia malalamiko haya.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kiutaratibu mstaafu anapostaafu tunatakiwa tuchukue miezi mitatu ili kuweza ku-process haki zake, lakini kuna baadhi ya nyakati huwa utaratibu wa miezi mitatu unaweza ukawa mkubwa zaidi kwa sababu ya nyaraka, nyaraka kutokuwekwa kulingana na viwango vinavyohitajika.

Kuna baadhi ya nyakati unatafuta nyaraka ya kuajiriwa inaweza ikachukua miezi sita haionekani nyaraka ile na lazima nyaraka zile zote ziwepo ili kuthibitisha kwamba kaajiriwa tarehe ile na cheti chake cha kuzaliwa kiwepo ili kuthibitisha kwamba umri wake wa kustaafu umeshafika. Ninachotaka kuwaomba ndugu zangu wanaosimamia uwekaji wa nyaraka za wafanyakazi ma-files yao katika wizara mbali mbali hawakikishe kwamba wanazitunza vizuri ili kuweza kumsaidia mstaafu kupata malipo yake katika kipindi cha miezi mitatu.

Mhe. Mwenyekiti, suala lake la pili nawaomba vile vile ndugu zangu wote wanaosimamia katika kuwalipa mafao wafanyakazi wanaostaafu waufate utaratibu huo. Lakini hata hivyo kwa wale ambao wana matatizo ya msingi na nyaraka zao wanazo na mpaka hivi sasa hawajapata fedha zao, basi vile vile nawaomba watumie fursa hii kuniletea nyaraka zao tuone kilichokwamisha ni nini.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri, kwa majibu yake fasaha na ya kina, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza (a) na (b).

- a) Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anisaidie kwamba kwa muda mrefu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumekuwa tukiitaka serikali iangalie upya viwango vya pensheni ambavyo wanalipwa wastaafu wetu, hasa wale ambao walistaafu miaka ya nyuma wakati malipo yalikuwa ya chini na matokeo yake mpaka leo yanawaathiri mno katika maisha yao ambayo gharama zake zinazidi kupanda kila siku. Sijui Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Umoja wa Kitaifa imechukua hatua gani katika kutekeleza kilio hiki cha wastaafu ambacho huwa kinawakilishwa hapa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.
- b) Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, anisaidie kwamba katika kipindi cha karibuni kumekuwa na taarifa ambazo hatimae zimepelekea hata Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulifanya kazi suala la wafanyakazi hewa ambao wanapelekea kulipwa mishahara hewa. Ni imani yangu kwamba ikiwa kuna wafanyakazi hewa wanaolipwa na mishahara hewa, inaweza vile vile ikapelekea kulipwa kiinua mgongo hewa na pensheni hewa. Sijui wizara yake imechukua hatua gani juu ya suala hilo.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** (a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nimepokea kupitia Baraza lako tukufu kwamba viwango vya pensheni viangaliwe. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi, kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilipoingia nadhani mwaka wa pili tu tumeviangalia viwango hivyo vya pensheni na tulianza kuvirekebisha. Lakini kwa sasa hivi ninavyokwambia ofisi yangu inaviangalia upya tena na panapomajaaliwa tunataki wenyewe tuvirekebishe kupitia bajeti inayokuja.

- b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli suala ambalo alilouliza Mhe. Mwakilishi kwamba kumekuwa na wafanyakazi hewa katika wizara zetu na taasisi zetu za serikali na tayari tumeshaona kwamba ufanyakazi hewa unatokana na nini, kwa sababu nikitoa mfano namkuta kijana anakwenda masomoni, barua yake inasema amepewa ruhusa miaka miwili, lakini miaka miwili imekwisha hajarejea na hakuna taarifa yoyote.

Hali hii tumeanza kuidhibiti na tutaendelea kuidhibiti ili wafanyakazi hewa wasikuwepo na malipo ya viinua mgongo hewa navyo vile vile visikuwepo. Naomba ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi katika eneo hili la upotevu wa mapato ya serikali tuendelee kusaidiana pale ambapo mtakapoona pana wafanyakazi hewa, basi tuarfiane ili twende tukafanye uhakiki wa kina na tuzuie huo uvujaji wa mapato ya serikali.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kuniona kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri, swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wafanyakazi wanapostaafu huwa kigezo kikubwa kinatizamwa umri wao tangu wanapoingia kufanya kazi. Na kwa kuwa anapostaafu anakuwa hana kazi tena pale anakwenda kuanza maisha mapya.

Je, kwa kuwa huyu anakuwa ni mzee ameshastaafu kwa uzee na serikali inawaweka muda mkubwa kuwalipa kiinua mgongo chao. Je, serikali kufanya hivyo haionti kama inawadumaza wale waliostaafu, kama ndivyo hivyo, serikali itafanya jitihada gani kuona kama inamaliza kuwalipa fedha zao wanaostaafu kwa sababu ndio wameshatoka kwenye kazi.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali sio kuchelewesha kuwalipa mafao wastaafu, lengo letu kuwalipa pale ambapo wanastaafu na muda umeshafika ili ziweze kuwasaidia katika kuendesha shughuli zao. Kama inatokea kuchelewa lengo sio la serikali kumcheleweshea, inawezekana kama nilivyosema kwa sababu ya nyaraka mbali mbali kuchelewa kupatikana, lakini tutajitahidi tuweze kuliona hili na kuwalipa kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao.

La msingi hapa nataka niseme mfanyakazi anapoajiriwa na yeye mwenyewe awe na utamaduni wa kuweka kumbukumbu zake, zitakapochelewa kule kumbukumbu zake angalau yeye anaisaidia ofisi yake kupeleka zile kumbukumbu ambazo hazionekani ili tuweze kutoa mafao yao kwa wakati.

## Nam. 92

### **Usumbufo kwa Watumiaji wa ATM**

**Mhe. Ali Salum Haji** - Aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara husika iliamua kulipa mishahara kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar ikianzisha utaratibu wa kutoa pesa kutumia *ATM* ili kuepusha misongomano siku za mwisho wa mwezi, lakini katika miezi ya karibuni *ATM* nyingi zinashindwa kutoa huduma kwa matatizo mbali mbali na kuleta usumbufo mkubwa kwa wananchi.

- (a) Je, tatizo ni nini.
- (b) Benki ya Watu wa Zanzibar imejipanga vipi kumaliza tatizo hilo.

**Mhe. Waziri wa Fedha** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- a) Mhe. Mwenyekiti, kushindwa kwa mashine za *ATM*, kutoa huduma hasa kwa siku za mwisho wa mwezi kunatokana na sababu zifuatazo:-
  - i) Mashine za *ATM* huwa zinafanya kazi kwa kiwango kila ifikapo mwisho wa mwezi, hali ambayo hupelekea kumaliza pesa mapema kabla ya muda wa uwekaji wa pesa. Aidha, wakati wa uwekeji pesa inalazimu *ATM* izimwe ili kuruhusu kazi hiyo kufanyika;
  - ii) Kukatika kwa mtandao wa mawasiliano (*Comunication Link*) kutoka kwa makampuni yanayotoa huduma hizo nayo pia ni tatizo ambalo husababisha mawasiliano ya *ATM* yasiwepo;
  - iii) Hitilafu za kiufundi kwa upande wa mtoa huduma wa mtandao (*Switch provider*) anaye unaiunganisha *ATM* na mtandao wa ndani za Benki; na
  - iv) Matatizo ya matumizi kwa baadhi ya wateja wanaotumia *ATM*, hali inayopelekea kadi ya mteja kukwama na kusababisha *ATM* kusita kufanya kazi hadi pale itakapotolewa na wahudumu wa benki.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Benki ya Watu wa Zanzibar imeshaanza kuchukua hatua kwa lengo la kukabiliana na tatizo hili, hatua zilizochukuliwa ni kama zifuatazo:-

- i) Kuongeza kiwango cha Bima katika *ATM* ili mashine ya *ATM* iweze kuruhusu kuwa na fedha nyingi zaidi;
- ii) Kuwa na mtandao wa akiba, ili pale inapotokea mmoja umekatika wa akiba uweze kufanya kazi; na
- iii) Kutoa elimu kwa wateja wa *PBZ* kuhusiana na namna bora ya utumiaji wa *ATM* pamoja na utunzaji wa kadi zao ili zisikwame katika *ATM*.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya ufasaha na yanayotoa matumaini, lakini pamoja na majibu yake Mhe. Waziri, nataka niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

- a) Pamoja na majibu yake ya matatizo ambayo yanaonekana ya kitaalamu ya kimtandao, ya watu kutokuwa na elimu ya kutosha, lakini na jengine la kutokuwa na fedha za kutosha, lakini bado inaonekana hata wingi wenyewe wa *ATM* katika Manispaa ni mdogo, tofauti na wenzetu ambaao wameweza kuonesha jitihada za kuweka *ATM* katika maofisi, kwa mfano *NMB* wameshawawekea polisi *ATM* yao. Na kwa kuwa Mheshimiwa mara nyingi tunatakiwa tutoe ushahidi na ushahidi wa picha sio tatizo la *ATM* ni tatizo la wingi wa *ATM*, yaani msongamano ni mkubwa wa foleni inakuwa mpaka Malindi mara nyingi hutwambia tutoe ushahidi. Je, ni lini *PBZ* wataanza kuweka *ATM* katika baadhi ya taasisi za serikali ili kuondosha usumbufu kwa wafanyakazi wetu.
- b) Pia, kwa kuwa tuna utamaduni na *PBZ* wameanzisha utamaduni wa kusafirisha pesa nje kwa kutumia utsaalamu wa *Western Union* na mara nyingi imekuwa inaleta usumbufu wa mitandao, hili nalo wanakabiliana vipi ili kuondosha tatizo hili.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubali kwamba tuna uchache wa *ATM* na nimelipokea wazo lake na shauri lake kwamba *PBZ* iangalie uwekaji wa *ATM* katika taasisi za serikali, nadhani wazo ni zuri ukiniuliza lini nitakuwa sina jibu isipokuwa wacha nilipokee halafu niweze kulifanyia kazi ili tuweze kuongeza *ATM*. Ukiangalia sasa hivi tumeweka *ATM* mbili katika jengo la *ZRB*, tumeweka *ATM* vile vile *Airport*, nadhani wazo hilo tutaliendeleza ili katika taasisi za serikali nako tuweze kuweka *ATM*.

Suala lake la pili sikuliskia vizuri naomba arudie.

**Mhe. Ali Salum Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuwa *PBZ* pia wameanzisha utaratibu wa kusafirisha pesa nje kwa kutumia utsaalamu wa *Western Union*, lakini pia, nalo tatizo hili la mtandao lilokuluwa linaleta usumbufu kwa wanaotaka kusafirisha pesa zao. Je, *PBZ* wamejipanga vipi kuondosha tatizo hili.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyo sema sasa hivi *PBZ* imeanzisha utamaduni au utararibu wa kuwa na mtandao wa akiba, kama mtandao mmoja utafeli basi mtandao mwengine uweze kufanya kazi na hizo ndio hatua ambazo wameshaanza kuzichukua.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, kuhusu suala la *ATM* nyingi hivi sasa zimejengwa katika Mkoa wa Mjini, ni lini serikali itachukua hatua ya kuweza kujenga *ATM* katika Mikoa ya mashamba ili kusaidia wananchi kwani wananchi wetu wengi wanaishi katika mikoa, wilaya hivi sasa pamoja na majimbo.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, hapa sitaweza kusema lini, lakini nalichukua wazo lake na pale ambapo tutakapoona katika maeneo ambayo kuna watu wengi wanahitaji kutumia *ATM* ili niwashawishi wenzangu wa *PBZ* waweze kuziweka katika maeneo hayo.

## Nam. 38

### Jitihada za Serikali kuwasaidia Wakulima

#### Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wazanzibari walio wengi wameelekeza maisha yao katika shughuli za kilimo, hususan kile kinachotegemea mvua za msimu, ambacho ndicho pekee kinachopunguza gharama katika uendeshaji wake. Na kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yamepelekea misimu mitatu ya mvua kwa mwaka yaani masika, vuli na mchoo ambayo haina uhakika katika upatikanaji wake na hivyo kwa kiasi kikubwa kuathiri maisha ya wakulima na wananchi kwa ujumla.

Je, ukiachilia mbali Serikali kuwataka wananchi wasiharibu mazingira, ni juhudi gani nyengine za Serikali zilizopelekwa kwa wakulima hao katika kuhakikisha shughuli zao za kilimo zinaendelea kuwa na tija kwao na taifa kwa jumla.

#### Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea kuwasihni na kuwataka wananchi kutokata misitu ya asili, uchimbaji wa mchanga ovyo na kuharibu mazingira kwani ndizo sababu za mabadiliko ya tabia ya nchi ambavyo husababisha kukosekana kwa mvua za msimu na kuathiri maisha ya wakulima na wananchi kwa ujumla.

Na athari ya ziada itafuatia baadae ikiwa wataendelea kukata hasa mikoko ambayo inazuwia upopo wa bahari na kupandisha kina cha maji, matokeo yake visiwa vitakatika vipande vipande na maji yatapanda mpaka viamboni na mfano hai hayo sasa yanatokea katika Kijiji cha Jozani na Mziwanda, Koowe na kwengine kwingi.

Juhudi mbali mbali zinafanywa na Serikali katika kuhakikisha kwamba inapunguza athari ya madiliko hayo kama ifuatavyo:-

1. Kuanzishwa kwa vikundi mbali mbali nya jamii kuhusika kwa matakwa yao wenye kuna misitu ya asili iliopo katika maeneo yao wanayoishi Unguja na Pemba;
2. Kutengwa kwa maeneo ya kulinda misitu ya asili, *project* ya *HIMA* chini ya ufadhili wa *CARE*;
3. Kufuata utaratibu wa kuutumia ukataji wa kuni kwa ajili ya matumizi ya majumbani;
4. Udhhibit wa misumeno ya moto usitumike mpaka kwa ruhusa ya kibali maalum;
5. Kufanya shughuli mbadala kama ufugaji wa nyuki katika zile sehemu ambazo misitu wa asili unatunzwa;
6. Mradi wa majiko sanifu ambayo yanatumia nishati kidogo;
7. Kutoa elimu ya ubaya wa kilimo cha kuchoma misitu na kuhama hama ambako kunasababisha kutengeneza jangwa;
8. Kutengenezwa kwa sheria ya kuzuia kukata miti ovyo (*COSMA*) zimetungwa ili kuthibiti wale wanaoharibu misitu;
9. Baada ya Sheria ya *COSMA* kutangazwa uongozi wa Serikali kupitia Wakuu wa Mikoa, Wilaya Maafisa Tawala na Watendaji wote wana taarifa pamoja na wananchi wote na vipi sheria zitaanza kutumika kwa wale watakaozivunja hatua zitakazochukuliwa; na
10. Elimu ya utunzaji misitu imetolewa kwa wananchi wale wanaoutunza msitu wenye na wanaozunguka maeneo yanayotunzwa. Kuanzisha utunzaji wa wanyama wa asili na kufanya uwindaji wa wanyama

wakongwe na kupata kipato kwa wanaotunza kwa kushirikiana na mfadhili wa *Wildlife Safari*. Kuandaa miti ya mikarafuu na kuwagawia bure wakulima, kupandwa miti katika sehemu zilizochimbwa mchanga au kifusi na kukatwa matofali.

Serikali ina mradi wa *TASAF* inaendelea na mpango wa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji. Wamesaidia umwagiliaji maji kwa kilimo cha mpunga na mboga mboga na matunda. Jumuiya kuhamasishwa kusafisha mitaro ili maji yasikwame na kusababisha maji kutotembea vizuri, pia kuzuia maradhi yanayosababishwa na kutuama kwa maji kama malaria na kichocho.

Kuwashajiisha wakulima hasa wa mpunga kupanda mazao yao mapema, kutumia mbegu bora za muda mfupi ambazo zinastahamili maradhi na mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo ukame na serikali imetoea ruzuku kwa mbegu, pembejeo na dawa za kuulia magugu.

Mashamba darasa kwa wakulima jinsi ya kulima kilimo bora kwa migomba na vyakula vya mizizi na jamii ya kunde. Wakulima waliosomeshwa njia bora za kulima na kuwapa fedha za kuanzisha mashamba kuitia mradi wa *PADEP* na *ASSP* na *ASDPL*.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa Wazanzibari hadi leo hii ni wapenzi wakubwa sana katika mambo ya wali, na kwa kuwa wanapenda sana mbegu zile za zamani ambazo zinahitaji maji mengi kama vile Mzuri hajipambi, Ringa, Kivuli, *Super*, Kihogo, Mpakulie bwana na kadhalika, ambazo mbegu hizi zinahitaji maji mengi na ambayo kwa sasa hayapatikani kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Je, kwa kuwa kuna *high bridge orison sativa 1164 aids*, hiyo *orison sativa KK11* hizi zinazaa kwa muda wa siku 35 tu, zinaota na kuzaa na kutoa mimea mizuri sana, wala hazihitaji maji mengi. Kwa kwa kuwa serikali mlituletea ile mbegu inayoitwa *Nerica haikufika* hata Vitongoji mbegu ile.

Je, ni lini sasa mtatuletea *orison sativa KK 11*, *orison sativa super 82* ili tuendelee kula wali kama tulivyozowea Wazanzibari.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa bado wizara yangu ina sehemu mbili; Kilimo na Utafiti na kwa kuwa bado suala la utafiti linaendelea kufanyika katika kutafuta mbegu bora ambazo zitazidi kuendelea na zinaweza kustahamili ukame. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi hiyo mbegu uliyoitaja nina imani ikiwa imo katika njia ya kufanyiwa utafiti ikishafanyiwa utafiti huo na ikiwa itatufaa basi mbegu hiyo italetwa wakati wowote.

**Mhe. Asha Abdu Haji:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa njia moja wapo ya usarifu wa mazao na matunda ni kuwa na vituo baridi. Je, wizara yake ina mpango gani wa kujenga vituo hivyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, hili swali liko kinyume na swali tuliloulizwa kuhusu usarifu wa mazao na kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa, lakini nitamsaidia kumjibu.

Mhe. Mwenyekiti, vituo vya usarifu wa mazao mpaka sasa hivi tunajenga. Tunalo jengo la Kizimbani na tumbakisha kulimalizia tu. Kwa hivyo, tumo katika *process* ya kujenga vituo hivyo vya usarifu wa mazao.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba ili kwenda na wakati na kulingana na hali ya mabadiliko ya hali ya hewa ni lazima tuweze kufanya tafiti mbali mbali, lakini taasisi ya utafiti ya Kizimbani ambayo iko chini ya wizara yake mara zote imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya fedha. Mimi kama mjumbe wa kamati tumeshuhudia kwamba hakuna tafiti zinazofanywa kwa sababu ya ukosefu wa fedha kwa taasisi hiyo.

- a) Je, mwaka huu wa fedha serikali itatenga fedha maalum kwa ajili ya kuwezesha taasisi hizo ili wananchi wajue maradhi ya matunda mbali mbali na mazao na ili wananchi wajitayarishishe na kuepukana na njaa.

- b) Mradi wa HIMA chini ya *Care* umekuwa ukitoa fedha kwa ajili ya kuwasaidia wana vikundi mbali mbali nya kuhifadhi misitu ya asili. Kwa nini sasa mradi huo hauombwi ukaeneza fedha hizo katika shehia zote za Unguja na Pemba ambazo zinahifadhi misitu hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe swali lake la pili sikumpata vizuri, lakini swali lake la kwanza kuhusu taasisi ya utafiti ni kweli ina changamoto ya fedha. Hilo tunakiri na wao wajumbe walipokuja hilo wameliona. Kwa hiyo, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutajitahidi kutenga pesa na wao wawakilishi waje watupigie debe ili fedha hizo tuzipate tuweze kuendeshea taasisi hiyo kufanya kazi kama ipasavyo.

Naomba swali la (b) arejee tena.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe naomba swali la (b) lirudie.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, swali la (a) niseme *Inshaallah*. Swali langu la (b) Mwenyekiti ni kwamba Mradi wa HIMA chini ya *Care* umekuwa ukitoa fedha nyingi kwa ajili ya wananchi wanaohifadhi misitu ya asili. Hoja yangu ni kwamba kwa nini mradi huo sasa hauhamashwi kusambaa shehia zote za Unguja na Pemba ambazo zimeathirika na wananchi wamekubali kupanda miti hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unahamasishwa pande zote, Unguja na Pemba na wakati ambapo tunapokuja kugawa fedha hizi mimi ni mmoja nimegawa fedha hizi walikuwa mpaka wananchi wa Pemba Jozani walikuja tukagawa kwa pamoja.

### Nam. 53

#### Wasanii Kupatiwa Mikopo

**Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-**

Wasanii wa Bongo Fleva kule Bara wamekuwa wakipanda chati kwa kiasi kikubwa na hatimae kujiongezea kipato kwa haraka sana. Kwa kuwa wasanii wa Zanzibar hawana “ma-promoter” pamoja na kukosa uwezo wa hata kwenda nje ya nchi kutayarisha kazi zao kama vile wanavyofanya wenzao wa Bara, jambo ambalo muziki wa “Zenj Fleva” pamoja na wasanii wake unashuka siku hadi siku.

Je, ni lini serikali itawapatia mikopo nafuu wasanii hawa au kuwapatia ‘Promoter’ kwa ajili ya kuendeleza vipaji na maisha yao.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 53 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa sasa haina mpango wa kutoa mikopo kwa wasanii kwa ajili ya kujitangaza, ila katika kuwasaidia *promotion* wasanii. Kwa jumla hapa Zanzibar na katika kukabiliana na changamoto zinazowakibili wasanii hao wa kizazi kipyaa na wasanii wa muziki asilimia, serikali inaendelea na mpango wake wa kuweka vifaa nya kisasa katika *studio* ya kisasa ya Rahaleo, itakayowezesha kurikodia kazi zao kwa bei nafuu. Kazi hiyo itaweza kuwatangaza wasanii hao ndani na nje ya Zanzibar na hivyo wasanii wetu waanze kutajika kulingana na vipaji na uwezo walionao nje ya mipaka ya Zanzibar.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wasanii katika nchi ya jirani tu hapo Tanganyika wanapata fursa mbali mbali kwenda kushiriki katika matamasha mbali mbali ya kimataifa na hivyo kuinadi Tanganyika katika medani za kimataifa. Mfano juzi tu Diamond alichukua nishani kadhaa kule pamoja na kina Ali Kiba, Lady Jaydee kwa kufanya kazi nzuri kuinadi nchi yao. Ni sababu gani za msingi Mhe. Waziri zinasababisha hawa vijana wetu wa Zenji Fleva hapa ambaa ni makini sana katika kunengua majukwaani na kutunga nyimbo kadhaa nzuri, wakashindwa kupata nafasi hizi na kuinadi Zanzibar kuititia wale wasanii asilia kina Bi Tele, Halikuniki, nk.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Mwenyekiti, jukumu la wasanii kwenda nje ya nchi ni namna ambavyo wenyewe wanaendelea kujitangaza na kuchangamkia hizo fursa. Kadiri watakavyoweza kujitangaza ndivyo ambavyo watapata fursa za kwenda nje ya nchi. Kwa ujumla wasanii wetu wanapata nafasi ya kwenda nje kujitangaza na kuitangaza nchi yetu, tukijaaliwa keshokutwa Ijumaa kuna kikundi cha wasanii 15 wataondoka Zanzibar kwenda Oman katika maonesho mbali mbali ya utamaduni.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya mwaka 2014

#### UTARATIBU

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie kifungu cha 63(1) cha kanuni zetu, kwa kuwa mara baada ya mswada huu kuwasilishwa hapa na Mhe. Waziri husika wa wizara hii, italazimika isomwe taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa kuwa katika kujadili mswada huu Kamati yetu tulikaa mpaka milango ya saa nne na nusu za usiku pamoja na mashirikiano makubwa waliyotupa viongozi wa kamati nyengine, tulifika karibu saa tano kasorobo. Kwa hivyo, ilikosa muda wa kutayarisha taarifa ya kamati na ndio tumo mbioni, iko kwenye *process* na sasa iko katika *final touches*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba huo nimelazimika kutumia kanuni hii ili uakhirishe Baraza lako hili hadi saa 11:00 jioni, kusudi mara baada ya kumalizika Mwenyekiti wa Kamati aweze kuipitia kwa umakini mkubwa taarifa ile, aje aieleze vizuri tena kwa muwala katika Baraza hili. Kwa hivyo, naomba sana Mheshimiwa utumie busara zako uakhirishe Baraza hili hadi saa 11:00 jioni, ili mswada huu uendelee na taarifa iliyo makini sana ya kamati yetu iweze kupatikana. (*Makofii*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe baada ya Mhe. Mjumbe hapa kwishakutoa hoja yake hii ni kweli kwamba jana tulifika saa nne na dakika kadhaa mswada ule ulikuwa ndio kwanza tunamalizia kazi ile, kiutaratibu kuna baadhi ya mambo hayajakamilika. Sasa ili wajumbe tuanze kuwapa *documents* ambazo ziko sawa na zinazoweza kusababisha kuchangiwa vizuri ni vizuri basi tukamuomba Mwanasheria Mkuu akatoa hoja ili baadae wajumbe wawewe kuiunga mkono na tuweke kanuni kando tuweze kusitisha shughuli zetu za Baraza kwa asubuhi hii hadi saa 11:00 jioni, ili tuweze kuendelea na taratibu zetu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mjumbe aliposimama alishatoa hoja, kwa hiyo sisi sasa ni kutuuliza tu iungwe mkono hoja hiyo, kwa mujibu wa kifungu cha 64 cha kanuni.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Haya tuwahoji wajumbe wanaokubaliana na hoja hii wanyooshe mikono. wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe sasa nachukua fursa hii kusitisha shughuli za Baraza letu kwa muda hadi saa 11:00 jioni, lakini tunaombwa kwamba tuhudhurie sote na kwa wakati. Ahsanteni sana.

*(Saa 4:36 kikao kiliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)  
(Majadiliano Yanaendelea)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikupongeze jioni hii ya leo wewe mwenyewe kuwa juu ya kiti pamoja na timu yako uliyoteremka nayo, hongera sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi pamoja na mambo yanayohusiana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kutayarishwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuanzishwa kwa Tume ya Maadili ni mionganini mwa azma ya utelezaji wa Sera ya Utawala Bora iliyopitishwa mwaka 2011 ambapo imetamka wazi wazi kwamba zipitishwe sheria maalum zitakazounda chombo huru cha kuzia rushwa pamoja na chombo cha kusimamia Maadili ya Viongozi. Ni dhahiri kwamba Sheria hii ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni moja katika alama muhimu za kukuza Utawala Bora nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria Maadili ya Viongozi ninaowasilisha mbele yako umezingatia maoni mbali mbali ya wadau wakiwemo wanasiwa, jumuiya za kiraia na wananchi kwa jumla.

Aidha, mswada huu ulipitishwa katika utaratibu wa kawada wa serikali ambapo umejadiliwa na Kamati ya Viongozi wa Wizara, Kamati ya Makatibu Wakuu na hatimae kujadiliwa na kujipitishwa na Baraza la Mapinduzi chini wa Mwenyekiti wake Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohd Shein.

Aidha, Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafasi hii maalum kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa uchambuzi wa kina wa mswada huu chini ya Mwenyekiti wake jamadari Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Wenyeviti akisaidiwa vyema na Makamu wake Mhe. Saleh Nassor Juma Muasisi Mwakilishi wa Jimbo la Wawi.

Kupata nguvu ya uchambuzi na kwa umuhimu wa mswada wenyewe kamati imejumuika pia Mhe. Mwenyekiti, pamoja na wenyeviti wengine wote wa kamati nyengine za kudumu za Baraza la Wawakilishi kuupitia mswada kwa pamoja, kwa wote sisi wizara tunasema ahsanteni sana na huu ndio moyo wa ushirikishwaji na kufanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, mswada wa sheria hii umeingiza mambo muhimu ambayo yanalenga katika kusimamia maadili ya viongozi ikiwa ni pamoja na kutaja maadili ya viongozi, miko na kuweka utaratibu wa kutangaza mali za viongozi. Kujipitishwa kwa sheria hii kutaimarisha utekelezaji wa Sera ya Utawala Bora na kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi.

Mswada huu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi umeweka msingi wa maadili ya kitaifa ambayo yanahitaji kutukuzwa na kulindwa. Msingi huo umetajwa katika jaduweli la kwanza. Sheria ya Maadili ya Viongozi itawahu Viongozi wote wa Umma wakiwemo watendaji wa serikali, Viongozi wa Kisiasa, watendaji wa Baraza la Wawakilishi na Mahakama walio katika nafasi za uongozi. Jaduweli la pili mswada linawataja viongozi wanaohusika na sheria hii.

Madhumuni na sababu ya mswada. Mhe. Mwenyekiti, ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi. Aidha, sababu nyengine za kutungwa kwa Sheria hii ni pamoja na hizi zifutazo:-

- Kuimarisha Utawala wa Sheria
- Uadilifu kwa Viongozi wa Umma
- Ufanisi
- Uwazi na Uwajibikaji wa Viongozi wa Umma
- Heshima na maadili mema kwa Viongozi wa Umma na Maadilifi ya Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Muundo wa Mswada. Mshwada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma una jumla ya vifungu 43 na umegawika katika sehemu kuu 7 kama ifuatavyo:-

- (1) Inaanzia kifungu namba 1 hadi kifungu namba 3.

Sehemu hii inazungumzia maelezo ya awali ikiwemo jina fupi la sheria pamoja na kuanza kutumika kwake. Matumizi ya sheria na ufanuzi wa maneno yaliyotumika katika sheria.

- (2) Inaanzia kifungu namba 4 hadi kifungu namba 14

Sehemu hii inazungumzia kuanzishwa kwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Muundo wa Tume, Uteuzi na Muda wa kushika Madaraka na Kinga kwa Mwenyekiti, Sifa za Mwenyekiti, Uteuzi wa Makamishina, Sifa za Kamishna, kula kiapo, wafanyazi wengine, kazi za Tume na Uwezo wa Mwenyekiti. Aidha, sehemu hii inazungumzia pia mashirikiano na taasisi nyengine.

- (3) Inaanzia kifungu namba 15 mpaka kifungu 21.

Sehemu hii inazungumzia maadili yatakayotumika kwa Kiongozi wa Umma. Miongoni mwa mambo yanayozungumziwa katika maadili hayo ni pamoja na kutangaza mali zinazopaswa kutangazwa, mgongano wa kimaslahi, kuzingatia miiko ya kijamii, Rais kukuza maadili katika Ofisi za Umma, uvunjaji wa maadili na kutovunja maadili.

- (4) Inaanzia kifungu namba 22 mpaka kifungu 29.

Sehemu hii inazungumzia utawala na utekelezaji ikiwemo daftari la kumbukumbu za mali na maslahi, malalamiko ya uvunjaji wa maadili, upatikanaji wa taarifa na ushahidi, ushauri wa kitaalamu katika utekelezaji wa madai au malalamiko, utaratibu wa kisikiliza madai au malalamiko, Tume kutoa maamuzi, ushahidi kutumika katika Mahakama na ripoti ya mwaka ya kazi za Tume.

- (5) Sehemu inaanzia kifungu namba 30 hadi kifungu namba 33.

Ambayo inazungumzia kuhusu makosa na adhabu ikiwemo hatua za kinidhamu. Makosa chini ya sheria hii, taarifa zisizo hasi na adhabu nyenginezo.

- (6) Inaanzia kifungu 34 hadi kifungu namba 37

Sehemu hii inazungumzia kuhusu masharti ya fedha ikiwa ni pamoja na bajeti na fedha za Tume, hesabu na ukaguzi, makadirio na ripoti ya mwaka ya fedha.

- (7) Inaanzia kifungu namba 38 hadi kifungu namba 43

Sehemu hii inazungumzia kuhusu masharti mengine ikijumuisha mamlaka ya mwenyekiti, kinga ya jumla, misngi inayopaswa kukuzwa na maadili, kanuni, marekebisho na kutangaza mali kwa Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa majaduweli mswada huu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma una majuweli 3. Jaduweli la kwanza linataja maadili ya viongozi. Jaduweli hili litasomeka sambamba na kifungu cha 40 cha sheria hii. Jaduweli pia linataja sehemu 6 ndogo nazo ni kama ifuatavyo:-

- (1) Kuweka na kukuza misingi ya maadili ya Viongozi wa Umma;
- (2) Umoja wa Kitaifa, Utawala wa Sheria na Kuheshimu watu wote;
- (3) Kuheshimu watu;
- (4) Kuzingatia tija;
- (5) Bidii ya kazi na;
- (6) Kuheshimu wadhifa alionao kiongozi. Vile vile ajira kwa mujibu wa sifa na mwisho zawadi ziwe kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi kila kiongozi wa umma anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

- (a) Aheshimu Sheria za nchi;
- (b) Aheshimu, asaidie na ateketeze maamuazi ya Mahakama na Mahakama maalum;
- (c) Ataheshimu na kufuata maelekezo halali na sera rasmi zilizoanzishwa;
- (d) Ataheshimu na kutekeleza sheria kwa kuitafsiri kila sheria kwamba imetayarishwa kwa maslahi ya umma na sio kuichukulia kwamba ni utaratibu tu au ni mbinu za kubatilisha adhma ya kutungwa kwa shheria hiyo;
- (e) Ataweka bayana udanganyifu, rushwa na ubadhirifu wa aina yoyote anao ufahamu.
- (f) Asitumie ushawishi kuweka shindikizo, kutishia au kuwadhalilisha watu wanaotekeleza majukumu yao kisheria na;
- (g) Asitumie vibaya kinga au fursa ya kisheria aliyonayo kama ni ngao au fursa au kufanya vitendo viovu ambavyo kwa nafasi yake jamii isingemtarajia kufanya hivyo.

Mhe, Mwenyekiti, katika kuheshimu wadhifa alionao basi kiongozi anapaswa kuheshimu misingi ya Utawala Bora kwa maana kwamba kutekeleza mamlaka yao na kufanya mawasiliano bila ya kificho; kwa uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji, mashauriano, kujiamini, haki na usawa.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi za Umma zipo kwa maslahi ya wananchi. Kwa hivyo, wenyewe dhamana ya taasisi hizo wanawajibika kuwatumikia wananchi ipasavyo. Vile vile uaminifu kwa wanaoshikilia uongozi katika Taasisi za Umma unaimairisha taasisi hizo na kukuza ufanisi unaotarajiwa. Pia, matumizi yoyote mabaya ya Ofisi ya Umma yanaharibu haiba ya ofisi na kuathiri uwezo wa mrithi wa ofisi hiyo kuwahutumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, jaduweli la pili linaonesha orodha za viongozi wa umma watakaohusika na sheria hii na jaduweli hili litasomeka chini ya kifungu cha 3 kilichotajwa kama kiongozi wa umma. Jaduweli la tatu limeweka fomu ya kutangaza mali na fomu ya malakamiko.

Kwa kuhitimisha Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe waujadili mswada huu, watushauri, watuelekeze na hatimae kumsaidia Mwenyekiti wa Baraza kupitisha kifungu kwa kifungu, ili iweze kutungwa na kupitishwa sheria ambayo itazidi kuonesha muelekeo wa nchi yetu katika suala zima la Utawala Bora nchini mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe baada tu ya kumaliza Mhe. Mwenyekiti, kutoa taarifa yake tutaanza majadiliano. Hivyo naomba wale amba wanataka kuchangia katika mswada huu waanze kuleta majina yao.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa):** Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe pamoa na Mhe. Spika, kwa kuweza kulisimamia Baraza hili vizuri na mpaka hadi leo tunaujadili mswada wa mwisho katika orodha ya miswada ambayo iliwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote tunaomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kwa kuweza kukutana hapa leo mbele ya Baraza lako Tukufu tukiwa wazima kabisa tena wenyewe afya njema, kwa lengo la kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake kwa ujumla, ikiwemo kupitisha miswada mbali mbali. Mswada huu ulio mbele yetu, Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na mambo yanayohusiana na hayo.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kuendelea kukushukuru wewe na ofisi yako kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuwasilisha ripoti hii kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Kamati, kuishukuru kwa dhati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Waziri Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, kwa kuweza kuona umuhimu wa kuleta mswada huu mbele ya Baraza ili uweze kujadiliwa na kupitishwa na kuweza kufikiwa lengo lilokusudiwa

la serikali la kuwa na sheria madhubuti itakayoweza kulinda Maadili ya Viongozi lakini pia kuwapa imani wananchi juu ya utendaji bora kwa viongozi wao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo Kamati yangu inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mara nyengine kupitia Mhe. Waziri kwa kuweza kushirikiana na kamati, lakini vile vile kwa kujadili mswada huu hadi jana saa 4:30 za usiku na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, leo tuliomba ofisi yako kwamba ituruhusu ili tupate nafasi ya kukamilisha ripoti hii na naamini Wajumbe wengi wameweza kuipata na ndio maana ukaona hata wamechelewa kuleta maombi kwa ajili ya kuchangia mswada huu.

Lakini naamini kwa kuwa wameshapata maoni ya Kamati lakini vile vile wameshasikia muhtasari ambao aliusoma Mhe. Waziri, naami Wajumbe wataweza kuwa na nafasi kubwa ya kuweza kuchangia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, dhana na maudhui ya Utawala Bora na Mswada wa Sheria hii ni kujenga jamii inayowajibika, yenye uwazi, inayoweka maslahi ya umma nje ya maslahi binafsi au ya mtu mmoja mmoja.

Aidha, sheria hii inalenga katika kuondosha upendeleo katika ajira, kupeana vyeo au nafasi yoyote ile ya madaraka kinyume na utaratibu uliowekwa kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati tulipokuwa tukiujadili na kuupitia mswada huu, ambapo tuliujadili bila ya kuchoka ili kuhakikisha kwamba lengo la mswada huu linafikiwa na hatimaye nchi yetu inakuwa na sheria madhubuti na itakayoteklezeka na itakayolinda Maadili ya Viongozi wa Umma hapa Zanzibar.

Mawazo na mapendekezo yao yamewezesha leo hii kufika hapa na kuweza kuwasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu na hatimaye kuptishwa kwa ajili ya kufikiwa lengo lililokusudiwa na serikali kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kama hivi ifuatavyo:-

1). Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2). Mhe. Saleh Nassor Juma	-	Naibu Mwenyekiti
3). Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
3). Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mjumbe
4). Mhe. Subeit Khamis Fak	-	Mjumbe
5). Mhe. Ashura Sharif Ali	-	Mjumbe
6). Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Mjumbe
7). Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu wa Kamati
8).Ndg. Makame Salim Ali	-	Katibu wa Kamati

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uzito wa Mswada huu na kutokana na mapendekezo ya ushauri wa Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Uongozi ilitupa kazi ya kushirikiana au ilitoa agizo la kushirikiana na Kamati ya Wenyeviti wote wa Baraza ukiwemo na wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti, ili kuukalia kwa pamoja Mswada huu kuweza kuujadili na hatimaye leo tumefikia kuweza kuwasilisha Barazani tukiwa na kauli moja ya kuunga mkono Mswada huu.

Naomba kwa ruhusa yako pia niwataje Wajumbe hao ambaa waliongezea nguvu Kamati yangu katika kuhakikisha kwamba Mswada huu mzito kabisa unapita katika Baraza hili la Wawakilishi.

Naomba niwataje Wajumbe hao ni:-

- 1). Mhe. Salmin Awadh Salmin
- 2).Mhe. Ussi Jecha Simai
- 3).Mhe. Omar Ali Shehe

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika Kamati yetu tulipata msaada mkubwa wa Mhe. Mwenyekiti - Mhe. Mgeni Hassan Juma ambaye ni wewe mwenyewe hapo, nadhani mchango wako katika Kamati uliweza kusaidia sana, bila

ya wewe siamini kwamba huu Mswada tungeliweza kuukamilisha kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuru sana kwa busara zako katika Kamati. (*Makofii*)

Vile vile, tulikuwa na Mwenyekiti mashuhuri, huyu ni Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni - Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na yeze alitusaidia sana katika Mswada huu na alitumia uzoefu wa kiti chako hicho kwa kweli kuhakikisha kwamba ule Mswada haulali na leo kuhakikisha kwamba unakuja hapa Barazani. (*Makofii*)

Pia, katika Kamati hii tuliongezewa nguvu ya Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, huyu alitusaidia sana kwenye Kamati ya ufundi na pale ambapo Mswada ulikuwa mgumu basi yeze alikuwa akisaidia sana katika mambo ya ufundi, ili kuhakikisha kwamba Mswada huu ulikuwa unapita bila ya matatizo yoyote.

Mwisho kabisa tulikuwa na Mhe. Abdalla Juma Abdalla ambaye na yeze ni Mnadhimu wa Chama cha Wananchi CUF ambaye pia alikuja kusimamia na kuhakikisha kwamba kwa kuwa yeze ni kiongozi Mnadhimu anasimamia kuhakikisha yale maadili yanasmamiwa na zile haki zote za viongozi zinaweza kusimamiwa vizuri, yeze ni Mwakilishi wa Jimbo la Chonga.

Kwa hivyo Mswada huu ni Mswada pekee ambaa umepata nguvu ya Kamati yenyewe ya Baraza lakini vile vile na Kamati ya Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi. Hivyo ninaamini Mswada huu Waheshimiwa Wajumbe wataujadili kwa nia moja na kuhakikisha kwamba unapita ili kuweza kuweka utawala bora katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo sasa naomba kuwatanabahisha Wajumbe kwamba marekebisho makubwa yamefanywa katika Kamati yangu, yamo kwenye orodha ya marekebisho ya Kamati ambayo tumegaiwa Wajumbe. Kwa hivyo hii ni sehemu ndogo tu ya marekebisho hayo ambayo orodha ya marekebisho hiyo ni sehemu ya ripoti yetu. Hivyo Waheshimiwa Wajumbe nitaomba pamoja na hii ripoti nitakayoisoma hapa, lakini kuna kile kiambatanisho cha marekebisho, naomba muweze kunukuu ili twende sambamba na Mswada huu ulivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo fupi sasa naomba nijielekeze kwenye marekebisho ya msingi yaliyofanywa na Kamati yangu kama hivi ifuatavyo:

Katika kifungu cha 29 kinachohusu ripoti ya mwaka ya kazi za Tume kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza maneno kwa mfumo wa kauli ya Serikali baada ya neno "kijacho" mwishoni mwa kifungu. Sababu ya marekebisho haya ilikuwa ni kuepusha kufunga mjadala juu ya ripoto ya mwaka ya kazi ya Tume ndani ya Baraza na badala yake kutoa nafasi tu kwa kuweza kuulizwa maswali Serikali juu ya ripoti hiyo itakayowasilishwa na Tume ya Maadili kwa kupitia kwa Mhe. Waziri hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, kama maelezo ya Serikali kupitia Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora aliyowasilisha hapa Barazani wakati akitoa hotuba yake, madhumuni makubwa ya Serikali kuleta Mswada huu ni kurejesha imani kwa wananchi kwa viongozi wao waliowachagua na wale waliopewa dhamana na Serikali kushika nafasi mbali mbali Serikalini, ili kujenga nidhamu, kuwa na maadili mema ya uongozi na dhamana walizopewa na kujenga uaminifu, kuondoa udokozi wa mali za umma, kuongeza uwajibikaji wa umma, kulinda na kuhifadhi mali na dhamana walizopewa na wananchi na Serikali kwa ujumla ili kuongeza ufanisi na kuleta maendeleo kwa wananchi wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu katika kurejesha nidhamu katika utumishi wa umma hapa Zanzibar hivi karibuni ililetu Sheria ya Rushwa na Uhujumu Uchumi hapa Zanzibar, jambo ambalo lilikuwa linaleta ukakasi katika kutekeleza sheria hiyo bila ya kuwepo kwa sheria hii ya maadili ya viongozi wa umma. Kwa hivyo kuleta kwa sheria hii kutaipa nguvu Tume ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama jadweli la pili la Sheria hii ya Maadili ya Viongozi, sheria inavyojieleza kuwa Mswada huu unawahuwa wakubwa na vigogo wa nchi. Kwa hivyo utekelezaji wa sheria hii unakuwa ni mgumu sana hasa kwa kuzingatia nguvu na sauti walizokuwa nazo katika nchi. Lakini pia uwezo wa kifedha walionao, sasa tujiulize hii Tume itakayoundwa ya maadili ni kweli itaweza kutenda haki katika kutekeleza uadilifu katika kutoa haki na kusimamia majukumu yao, bila ya kuingiliwa katika maamuzi yao.

Isitoshe Mhe. Mwenyekiti, je, tujiulize ni kweli Tume hii itaweza kuibua mizengwe iliyofanywa na inayofanywa na viongozi ambao waliopo madarakani na wale waliostaafu ambao hadi leo wanashikilia mali za umma na haki za wananchi wengine wanyonge. Sasa kwa maoni yangu Tume hii imepewa mtihani mkubwa na sijui kama kweli wataweza kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu unaostahili. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikasema hivyo? Wananchi wengi ambao ni wadau wakubwa katika sheria hii hivi sasa wanaisubiri kwa hamu sheria hii ili kuwaburuza wakubwa na vigogo kwenye Tume ya Maadili, ili kudai mali zao zilizochukuliwa kwa nguvu na kwa kutumia mamlaka waliyopewa na wananchi.

Wengine wanaotumia nyadhifa zao kwa kuwanyang'anya mali zao na kuwapa aidha marafiki zao au watoto wao au ndugu zao. Kwa hivyo, kwa sheria hii vigogo hao wajiandae kuburuzwa kwenye Tume ili kuweza kujibu mashitaka yatakayopelekwa na wananchi dhidi yao na pia tutaangalia ikiwa Tume itaweza kutumia madaraka iliyopewa na sheria hii, kuweza kutoa ushauri kwa mamlaka husika kwa kuweza kurejeshwa wanyonge haki zao. Pia kurejeshwa kwa mali za umma zinazomilikiwa aidha na viongozi au waliokuwa viongozi walipokuwa madarakani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Serikali katika sheria zote ilizozileta hapa Barazani, hii ndiyo sheria ya mwanzo ngumu katika utekelezaji wake. Kwani Mhe. Rais atakuwa na mtihani mkubwa wa kutoa maamuzi magumu kwa wale wateuzi wake aliowapa dhamana ambao ni wengine wapambe wake, wengine ni marafiki, wengine ni ndugu zake, jamaa zake na wakati mwengine hata ye ye mwenyewe, kwani sheria hii inagusa wakubwa watupu. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, sheria kama hii ndiyo iliyomfanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweza kufanya mabadiliko makubwa kwenye Baraza lake la Mawaziri kwa zaidi ya mara tano katika kipindi chake cha uongozi wa miaka kumi akiwa mkuu wa nchi. Mfano mzuri wa matokeo yaliyojitezea hivi karibuni katika kadhibya fedha ya akaunti ya *Escrow* kule Tanzania Bara ambapo karibu Mawaziri mawili na baadhi ya watendaji wa Serikali waliwajibishwa kuititia Sheria ya Maadili ya Viongozi, kwa ushauri na mapendekezo ya Tume ya Maadili ya Jamhuri wa Muungano. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, ndiyo maana tukasema hii ndiyo sheria ngumu ya mwanzo katika utekelezaji wake kwa hapa Zanzibar. Kwa hivyo Kamati yangu inatoa wito kwa wale waliopo karibu na familia ya Mhe. Rais, Mawaziri, Majaji, Wawakilishi na viongozi wengine waliotajwa kwenye Mswada huu na wale wote walipewa dhamana, aidha Serikalini au walipewa dhamana na wananchi kujirekibisha makosa yao, na kama wapo waliochukua mali za watu wazirejeshe kabla ya Mhe. Rais kuutia saini sheria hii. Vyenginevyo sheria hii itakuja kuwaumbua. (*Makofî*)

Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba sana Serikali yetu hasa kupitia kwa Mhe. Rais asiwafumbie macho wale wote watakaopelekwa kwake, ambao watagundulika wamevunja maadili ya uongozi kwa kuwachukulia hatua za kisheria kwa haraka, ili kujenga imani kwa wananchi wetu. Kwani hivi sasa kupitia ripoti mbali mbali za Kamati Teule zilizoundwa na Baraza la Wawakilishi na kutolewa ripoti hapa Barazani, lakini utekelezaji wake umekuwa ukisuasua pengine kwa udhaifu wa kisheria. Kupitia sheria hii, ninadhani tutakuwa tumekupa nguvu sasa ya kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale wote watakaohusika.

Mhe. Mwenyekiti, pia labda kama kuna viongozi ambao bado wapo madarakani ambao wamesababisha wananchi kukosa haki zao kwa kuwapa watu wengine, kuwapa jamaa zao au rafiki zao au kuzichukua wao wenyewe, kwa hivyo pia kupitia Mswada huu sasa ni wakati wa kujisafisha kwa viongozi wote wa umma hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mswada huu katika kifungu cha 15 kinachoelezea viongozi kutangaza mali zao, wao wenyewe na familia zao na baada ya kushika madaraka na pia kila baada ya mwaka mmoja na wakati wanapoondoka madarakani, ili kumfanya kiongozi wa umma aaminiwe na kukubalika kwenye jamii.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mswada umeelezea kiongozi kueleza ukweli mtupu katika kutangaza mali zao na ikitokezea kudanganya itakuwa ni kosa na hatua za kinidhamu na kisheria zitachukua mkondo wake. Sasa kwa kifungu hiki tutaangalia ukweli wa viongozi ambao tukiwemo na sisi katika kutangaza mali zetu, kwani kuna baadhi ya watu wenye dhamana wanamiliki mali ambazo hata ukifanya tathmini ya kipato chao basi hawawezi kumiliki mali hizo. Sasa suala hili itakuwaje?

Mhe. Mwenyekiti, Tume itachukua hatua gani kwa wale watakaogundulika wamemiliki mali kinyume na uwezo wao kisheria. Kwa hivyo wananchi wanasubiri kwa hamu Tume hii jinsi itakavyoweza kuibua mambo ya namna kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mswada huu umeelezea kiongozi au mtumishi awe muaminifu katika dhamana aliyopewa na wananchi au Serikali. Lakini suala hili limekuwa sugu Serikalini, kwani kwa nyakati tofauti tumesikia watu kuiba mali za umma zikiwemo nyaraka za Serikali, pesa taslimu na hata baadhi ya thamani za maofisini.

Kama hiyo haitoshi kumekuwa na kadhia kubwa kwa uvujaji wa mapato ikiwemo kwa malipo yanayolipwa au yaliyolipwa kwa wafanyakazi hewa amba Baraza lako Tukufu limemtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulifanyia uchunguzi suala hili, lakini cha kushangaza na cha kusikitisha hadi leo hii hatujaletewa ripoti hii hapa Barazani. (*Makofisi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo kupitia sheria hii tunamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutuletea ripoti hiyo ya uchunguzi ili tuweze kuiagiza Serikali kuwachukulia hatua kali za kinidhamu wale wote watakaobainika na upotevu wa pesa hizo na wazirejeshe Serikalini, kwani huo ni ukiukwaji mkubwa wa maadili ya viongozi wa umma na utumishi wa umma kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaamini baada ya kupitishwa sheria hii, kuna baadhi ya viongozi na hata watendaji wataamua wao wenye kusamehe nyadhifa zao ili sheria hii isiwakumbe, kwani itakapokuja kwani sheria hii itakuja kuwaumbua. Lakini pia waliobaki wataongeza bidii katika utendaji wa kazi zao kama kifungu cha 16 cha jadweli la Mswada kinavyoolezea.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika sheria hii kifungu cha 17 kimeelezea kuhusu kiongozi kuepuka kuweka maslahi binafsi katika utumishi wa umma. Mhe. Mwenyekiti, bila ya kificho tatizo hili limekuwa ni kubwa katika Serikali yetu, kwani kuna baadhi ya watendaji au viongozi amba hutumia nyadhifa zao kwa kutumia mali za umma kwa kuzalishia na kujilimbikizia mali wao wenye binafsi na mifano imo kwenye ripoti ya Kamati Teule za Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, wengine hutumia taarifa na mipango iliyokuwemo kwenye Wizara zao kwa kijiandaa aidha kujipatia tenda au kujipatia biashara kupitia mipango ya Serikali, jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa sheria hii. Suala hili ni kubwa na ukiukwaji mkubwa wa maadili lakini pia suala la maslahi binafsi linalosababisha hata baadhi ya miradi ya Serikali kuchelewa, na pia kukosa viwango na ubora unaostahiki. Kwani kwanza wakubwa huchagua kampuni za marafiki zao na kuwapa kazi ambazo aidha hawana uwezo nazo ama huchukua rushwa ili kuweza kuwapatia tenda.

Pia, wakati mwengine kuna viongozi huamua kwa makusudi kulazimisha kukiuka kwa baadhi ya maamuzi ya *Tender Board* katika kutoa *tender*, ili wapewe makampuni yao au jamaa zao ili na wao waje kufaidika na miradi hiyo kama katika mifano hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sisi kama Wajumbe tutakuja kuitumia sheria hiyo kuja kupinga kampuni ambazo zitapewa kazi ambazo hazina uwezo hapa Barazani, ili kazi hizo wapewe zile kampuni zinazoshinda kisheria, kwani tumechoka na miradi ambayo isiyokuwa na viwango.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii pia imeelezwa kuwa kiongozi hatopokea zawadi akiwa katika utumishi wa umma, isipokuwa zawadi hiyo itakuwa ni mali ya umma na atatakiwa aiwasilishe Serikalini. Suala hili ni geni hapa kwetu Zanzibar, kwani tumezoea kuona na kusikia viongozi wetu tukiwemo na sisi kupewa zawadi mbali mbali za nje na ndani, wakati mwengine zawadi hizo haziletwi Serikalini lakini viongozi huzitumia kwa kujinufaisha wao binafsi.

Wakati mwengine wale wanaotoa zawadi hutoa kwa ajili ya kuwashawishi viongozi hao kuja kufaidika na miradi au biashara zao. Kwa hivyo, tunatoa tahadhari kwa viongozi sote, wakubwa au wadogo kujiepusha kuanzia sasa kupokea zawadi ambazo zitakazowasababisha kutoa upendeleo kwa watu wao, na hivyo kwa hivi sasa tunatakiwa tuwe makini katika kupokea zawadi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, katika mswada huu kumetajwa suala la kuepuka kutoa upendeleo katika masuala mbali mbali likiwemo suala la ajira. Mhe. Mwenyekiti, eneo hili pia ni kubwa na tunatakiwa kuchukua tahadhari kuanzia hivi sasa, kwani wakati mwengine sisi wakubwa hutoa vimemo kwa taasisi zinazotoa ajira ili watu au jamaa zao waweze kupatiwa ajira, hata kama hawana sifa na uwezo wa kuajiriwa katika sehemu ile. Ndio maana tukasema hii ni miongoni mwa sheria ngumu kuitekeleza hapa Zanzibar, kwani kutoikutii maagizo ya wakubwa kunaweza kukapelekea kuhatarisha ajira za hao wanaopelekewa vimemo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo kwa kuwa sheria hii ni msumeno basi tuijandae na changamoto zake, kwani tatizo la Zanzibar ujomba tumeuweka mbele kuliko sifa na uwezo wanaopewa dhamana katika kazi, kwani wakati mwengine bila kificho kuna watu hupewa dhamana kubwa serikalini wakati hawana uwezo wa kazi hizo na kupelekea kuikoseshaa serikali huduma bora na kuchelewesha kazi ya maendeleo katika taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya wananchi hawana uwezo nayo kwani yako katika mamlaka za uteuzi, jambo ambalo linadharaulisha serikali kwa jamii. Kwa wakati mwengine wale wanaopewa dhamana hizo huzitumia vibaya, kwani wanajua wanalindwa na wakubwa waliowapeleka katika nyadhifa zao hizo na kupitia migongo yao.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu pia umeelezea matumizi mabaya ya madaraka, matumizi mabaya ya mali za umma, ikiwemo matumizi ya magari ya serikali, lakini pia nyumba za serikali, kwani kuna magari ya serikali hutumika baada ya saa za kazi na utawakuta watu wanayatumia kwa shughuli zao binafsi, bila hata kibali cha serikali au kutoka kwa wakubwa wao.

Pia kuna baadhi ya watu waliokuwa viongozi hadi leo wanazitumia nyumba za serikali kinyume cha sheria na serikali imekaa kimya na hatuna hatua zozote za kisheria zinazochukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika nyumba hizo kuna baadhi yao wamefikia hatua za kuwarithisha jamaa zao. Sasa hebu tuijulize je, ikiwa kila kiongozi au mtumishi aliyepewa kutumia nyumba ya serikali kama hataki kuirejesha, je nyumba hizo zitabaki serikalini au kuna sheria gani ya kiongozi kugaiwa nyumba ya serikali. Ndio maana pale mwanzo nikasema sheria hii itakuwa ni ngumu katika kutekeleza, hasa kwa muhali ambaa tumezoweaa kuchukuliana hapa Zanzibar.

Lakini kwa kuwa sheria ni msumeno hatuna budi sote kwa pamoja tushirikiane katika kuitekeleza sheria hii, hayo ndio maadili ya kila aliyekubali kuwa kiongozi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu namba 2 cha jadweli la pili la mswada huu, umeelezea viongozi kuheshimu sheria, utawala bora na kuheshimu wananchi wote kwa ujumla. Pia kuheshimu taratibu za kubadilishana madaraka katika chaguzi mbali mbali, kuheshimu uhuru wa mahakama na kuwa na serikali siki na pia umoja wa kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuheshimu uhuru wa mahakama, lakini pia mahakama zenyewe kuwa na uadilifu katika kutoa hukumu ili kulinda maadili ya mahakama pamoja na mahakimu wenywewe.

Vile vile kujiepusha na kuvunja sheria na kutoa maamuzi yasiyo ya haki hasa kutokana na nguvu ya kisheria, kwani tumeshuhudia kuwa kesi nyingi hasa za ubakaji na madawa ya kulevyaa zimekuwa hazipati hukumu ambazo wananchi wengi wamekuwa wakizitarajia, jambo ambalo huwafanya wananchi kukosa imani na vyombo vyetu hivi nya kusimamia haki.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kifungu cha 7 cha jadweli la kwanza la mswada huu, kinachoelezea kuwa serikali itakuwa na jukumu la msingi la kuheshimu na kutekeleza maazimio ya vyombo vyetu kutunga sheria, yaani Baraza la Wawakilishi. Kwa kifungu hiki sasa tukiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakuwa na haki ya kuidai serikali utekelezaji wa maamuzi halali ya Baraza lako kila pale tunapoyapitisha.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumaliza hotuba yangu, Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe japo dakika tatu au nne kuweza kutoa maoni binafsi nikiwa kama Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe, sheria hii ni sheria ya aina yake. Sheria zote ambazo tunazipitisha hapa Barazani zinawagusa mpaka wauza kuni, wauza mchicha, wauza madagaa, yaani nakusudia wale

watu wa hali ya chini. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sheria hii inaanza kungusa kiongozi mkuu wa nchi, mpaka ngazi fulani ya uongozi tukiwemo na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, wakati umefika kabla Mhe. Rais kuitia saini sheria hii tuanze kubadilisha tabia, tuanze kujirekebisha kama tulikuwa tuna mambo yetu tuangalie majadweli yanasema nini, tunabanwa katika miko gani katika sheria hii.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri kama nilivyosema mionganoni mwa sheria ngumu tulioipitisha katika Baraza la Wawakilishi ni sheria hii na kwa kweli ni watu wa ajabu sana serikali ya Awamu ya Saba, kuweza kuamua kujifungia ndani na sheria hii ambayo na sisi wenyewe sote inatukumba, lakini kwa ujasiri wenu mumeweza kuileta hapa Barazani. (*Makofsi*)

Kwa hivyo, kitu ambacho ninachokuomba Mhe. Waziri kutoa semina, kama kumefanyika semina bado hii sheria watu walikuwa hawajajua au hawajaamini kama sheria hii itakuja, kutoa semina watu wapate fursa ya kuuliza.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ina majadweli mengi, majadweli hayo yote yanahusu tabia za viongozi. Sasa na hatua hii tuliyofika sasa hivi tunakwenda katika kipindi cha uchaguzi. Kama ungeniuliza mimi Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Rais sheria hii akaitia saini mwezi wa Julai, pale tunaaga aitie saini sheria hii, ili atakayekuja kukabidhiwa uongozi basi kwanza asome sheria hii na majadweli haya, halafu ajipime ninayo sifa ya kuwa kiongozi. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, nina wasi wasi sheria hii ikitiwa saini katikati ya kipindi hicho, kwa kweli itakuja kuwa hatari kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba sasa hivi wananchi wameamka, wananchi wanajua haki zao na wanajua kuzidai. Mara nyigi ukiangalia mfano kama wenzetu Tanzania Bara, mara nyigi wana harakati sheria kama hizi ndio wanazifanya kazi. Mwenyekiti wa Tume atakuwa na foleni kubwa kwa wanaharakati na kwa wananchi wa kawaida, wanakwenda kushtakiwa wakubwa. Sasa kipindi kama hiki na tafrani ya kuitwa katika Tume na huku jimboni tayari mambo yanaanza. Lakini kwa kuwa tumekubali utawala bora basi hatutaki kumfunga Mhe. Rais kuweza kutekeleza ile nia yake ya kuhakikisha kwamba amekabidhiwa madaraka na Wazanzibari na atatenda haki, ili kuhakikisha kwamba viongozi wote wanahestimiana na wanahestimu mpaka mtu wa chini.

Kwa hivyo, kama tulivyosema, tunaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuisome vizuri sheria hii, majadweli haya tuyasome vizuri mtu kila ambapo atakuwa na swalii, amuuilize Mhe. Waziri. Kama cha kukiondoa tukiondowe hapa na kama cha kukibakisha basi tukibakishe hapa. Tukija tukikosea hapa, Mhe. Mwenyekiti, Tume kama hii ina nguvu kubwa.

Sisi tulikwenda kule Tanzania Bara Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ile Tume ina nguvu kubwa, watu wanasiakia tu aah Mhe. Rais amefanya mabadiliko. Zile ni ripoti za Tume, Mhe. Rais hakai tu akakurupuka akasema anafanya kitu fulani. Mtasema kwenye Bunge, mtasema kwenye Baraza la Wawakilishi, lakini jambo ambalo linahusu maadili basi Mhe. Rais mara nyingi anasubiri ripoti ya Tume.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, sijui Mhe. Waziri kama ameshanusa nusa nani atakuwa Mwenyekiti wa Tume hii, lakini kwa kweli Mwenyekiti huyu tutaomba sana apewe ulinzi wa kutosha. Vile vile apewe uhuru wa kuweza kufanyakazi yake. Lakini kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, Tume hii tusije tukaifanya kama Tume nyengine.

Tume inaundwa haina vitendea kazi, haina ofisi. Ndio maana nikaomba serikali yetu kama hatujajitayarisha vizuri, basi sheria hii icheleweshwe kidogo kutiwa saini, ili Mwenyekiti wa Tume achaguliwe mtu ambaye yuko makini na apewe nyenzo za kutosha katika kufanya kazi vake.

Mhe. Mwenyekiti, Tume hii baada ya kuundwa ikiwa hajapewa nyenzo, basi tutakuja kuilaumu hapa Barazani. Kwa sababu Tume hii inapotaka kumchambua mwakilishi, kama ana mali zake Comoros, kama ana mali zake Dubai, kama ana mali zake Oman, kama ana mali zake Wete, pahala popote Tume iweze kuwa na uwezo wa kwenda kuzifua tilia na kuhakikisha kwamba mheshimiwa kile alichokijaza katika fomu ni kitu cha kweli. Vyenginevyo, kusema kwamba Tume hii inapewa bajeti ambayo mafuta yao hata wakitembea katika kisiwa kimoja tu cha Unguja pengine wasikimalize mafuta yamekwisha.

Kwa kweli Tume hii itakujakuwa kama *white elephant*, haitoweza kufanyakazi zake vizuri. Tume hii ndio itakuwa kivoo cha utawala hora wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache, namshukuru sana Mhe. Waziri. Lakini namkumbusha tu ile ahadi yake ya kutoa mafunzo zaidi kwa wajumbe wa kamati, ili kujifunza kwa wenzetu ni namna gani Tume hizi za maadili zinavyofanyakazi na sheria hii inavyofanyakazi. Basi ninaamini Mhe. Waziri ataweza kutekeleza ile ahadi yake na ninaamini kipindi kilichobakia hicho basi atajitahidi ili kuhakikisha kwamba wajumbe wanapata uelewa mzuri zaidi katika maadili ya viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, na kwa niaba ya wajumbe wangu wa kamati naomba kuunga mkono hoja. Naomba Mhe. Mwenyekiti, wajumbe usiwabane kwa sheria hii, wajumbe wape nafasi wachangie na waulize maswali kwa sababu hii sheria inawhusu wao, tofauti na sheria nyengine. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. (*Makofsi*)

**Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali:** Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa pumzi ya kuweza kuwepo hapa.

Nichukuwe nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, kaka yangu pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye aliyemaliza kutusomea taarifa hizi. Mhe. Mwenyekiti, labda niseme jambo moja tu.

Humu ndani Mhe. Mwenyekiti, tumekuja kwa niaba ya wananchi na tumekuja kutekeleza yale ambayo wananchi wametutuma kuja hapa. Mhe. Mwenyekiti, sheria hii sio ngumu na inanipa tabu sana, nia ipo? Kwa sababu tunaposema maadili, nchi yetu hii ya Tanzania tuliyonayo sasa hivi, maporomoko ya maadili ndio yaliyotufikisha hapo tulipofika. Nasema haya kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tulishuhudia hivi karibuni kwenye Bunge watendaji wameingizwa mabilioni ya pesa ndani ya *account* yao. Kubwa anaambiwa mtu ajiuzulu, mtu kaingizwa mabilioni kama njugu na kakaa kitako anazunguka. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hivi nia tunayo ya kuyafanya haya, maana tutakuja tuyapitishe haya, lakini yana mambo yake Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, ninachosema mimi mkazo wangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa hali hii tunayokwenda nayo, iwe tumekubaliana na nia iwepo. Nina mifano hai Mhe. Mwenyekiti. Haya yote tunayozungumza sasa hivi ni mambo ya maadili na yanawagusa viongozi wote karibu 79 katika sheria ya maadili. Lakini Mhe. Mwenyekiti, humu ndani tumeshuhudia mambo mengi kamati nyangi zimetoa ushahidi, zimetoa hoja na maporomoko ya maadili hakuna kilichokuwa kimetekelezwa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, lengo langu kubwa mimi ni kusema kwamba kiwepo na kifungu cha kuwa kiongozi yejote au mtendaji yejote, panapovunjwa maadili basi iwe siku ile hayupo kazini, halafu sheria ichukuwe mkondo wake. Lakini utamkuta mtu keshangiziwa bilioni mbili keshaitia serikali hasara na bado yupo.

Kwa hivyo, mimi ninachotaka kusema ni kwamba suala la urafiki, suala la udugu, suala la kuwa swaiba wako ndio linalotufikisha hapa tulipofika. Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza suala hili la *Escrow* ambalo lilikuwa Bungeni kule, huo ni ushahidi wa wazi upo. Lakini vile vile katika Baraza hili lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, ambalo tuko hapa, kulikuwa na baadhi ya mawaziri walikuwa wanazungumza kitu ambacho tuna ushahidi, mimi nina ushahidi kwamba wamekuwa sio wakweli, hayo ni maporomoko ya maadili. Anakuja mwakani anazungumza kama sio yeje.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, *are we serious?* Kwa sababu tumeyashuhudia haya yana ushahidi mkubwa, kwamba baadhi ya watendaji, baadhi ya mawaziri wamekuwa sio wakweli na ushahidi upo, hata nikiambiwa kesho mimi nitatoa ushahidi. Wanakuja wanaudanganya umma wazi, mchana na serikali inajua hakuna utekelezaji wowote unaofanywa na anakuja mwakani anazungumza kile kile, alimradi tu wawakilishi tunazuwia vifungu, baadhi ya mawaziri wanasmama wanawapigia kifua na matokeo yake wanasema ah! tumeshamaliza ngoma. Sasa Mhe. Mwenyekiti, maporomoko haya ya maadili ni lazima tuyatizame kwa njia zote.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nina ushahidi serikali imeridhia madeni mengi sana katika Awamu hii ya Saba ambayo inaongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Al-Hajj Dk. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu leo inadaiwa mamilioni ya dola na kwa sababu tu baadhi ya watendaji kutokana na ubinaksi wao, umimi umimi, makampuni yamekwenda mahakamani, watendaji waliitwa mahakamani. Matokeo yake kwa sababu watendaji wameshaona mimi ni mteuliwa wa Rais itakuwa nini, kwa hivyo hajui sheria wala

anaona ile mahakama ni jambo la kawaida. Matokeo yake Mhe. Mwenyekiti, leo Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inadaiwa mamilioni ya dola.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa jitihada zake za kuwatuma baadhi ya mawaziri kwenda kulifanyia kazi hili, ili deni hili kulisawazisha. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, haya yote ni maporomoko ya maadili serikali yetu hai hoi. Kwa hivyo, mimi ninachosema Mhe. Mwenyekiti, mkazo wangu ni kwamba haya mambo tunakuwa tunayazungumza na tumo humu ndani kuyajadili, nia ipo ya utekelezaji?

Mhe. Mwenyekiti, katika yote haya utakuta maadili ya sheria ukurasa 62, kifungu 28 naomba ninukuu;

"Bila kuathiri sheria nyengine ushahidi utakaotolewa mbele ya Tume utatumika kama ushahidi mahakamani".

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini sisi Baraza la Wawakilishi tunatoa ushahidi hapa usitumike mahakamani, hii hapa. Yaani mbele ya Tume kama ushahidi utakuwa umesomwa, ukienda mahakamani ile Tume utatumika ushahidi wetu. Sasa sisi Baraza la Wawakilishi hapa tunatoa ushahidi na tunapokea ushahidi na tunatoa vielelezo. Kwa hivyo, mimi naona na hili Baraza la Wawakilishi ushahidi huu utumike mahakamani vile vile. Mhe. Mwenyekiti, nimeona hili ni jambo ambalo tusaidiane katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi sina zaidi ya kusema, naunga mkono hii sheria ya maadili, lakini Mheshimiwa hapo tulipofika ni maporomoko tu ya maadili na haya yanaendelea bado, na kwa kweli kama sio ustahamilivu utakuta Serikali yetu imeingia hasara mabilioni mpaka leo kwa sababu tu watendaji wameteuliwa na Rais hakuna utekelezaji kila mtu mbabe. Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo watu watakwenda kudai haki basi Mahakamani patakuwa hapatoshi mpaka Dar es Salaam kwa foleni.

Sasa mimi ninachotaka kusema Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba uongozi ni hekima, uongozi ni busara na uongozi ni usikivu, kwa hivyo mimi nilitaka kuomba kwamba watendaji tuwe na dhamana katika nafasi zetu tunazopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napongeza hatua hii iliyochukua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuleta Sheria ya Maadili ya Viongozi, lakini nataka kusema tu kama nia ipo na hili Baraza tushashuhudia mambo mengi, matumaini yangu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu basi tusiandikie mate wino upo, tuje na hili tuliunge mkono na mimi naliunga mkono, kwa hivyo kinachofuata Sheria, Sheria, Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kukushukuru kwa niaba ya wananchi. (*Makofit*)

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti kunipa fursa na mimi jioni hii ya leo kuchangia mswada huu mzuri wa maadili.

Mhe. Mwenyekiti nimi ni mjumbe wa Kamati hii ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na huu mswada kwa kweli ukiutizama kwenye maudhui yake ni mzuri sana, lakini Mheshimiwa kwa kweli tatizo ni utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kila siku nikichangia nasema na leo nitasema tena kama Zanzibar kwa kutunga Sheria nzuri hatushindwi, lakini tatizo ni utekelezaji wake na tatizo linakuja kwa sababu hatuko wakweli kabisa, tunatunga Sheria nzuri tukishazitunga Sheria nzuri tunaziweka ndani ya pakacha hatufuati zile sheria sasa zile sheria zetu tunazotunga wenywewe hatuzifuati.

Mheshimiwa hili mimi linanisikitisha sana, kuwa tunatunga sheria lakini kuzifuata sheria hatuzifuati, Mheshimiwa Sheria hii ya maadili inafuatana na vitu vitatu ambavyo vinalingana ili sheria hiyo ya maadili itekelezeke; kwanza zinatakiwa haki za binaadamu ziwe zinaheshimiwa, halafu utawala bora uwepo na utekelezwe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema ukweli hii sheria uzuri wake iliyonao lakini ni sheria ngumu kweli kweli, na hii sheria ingekuwa kweli kama hivi ilivyoandikwa humu itatekelezwa basi Zanzibar tungekuwa tuna viongozi wazuri kweli kweli, lakini Mheshimiwa nyote ni mashahidi nyinyi kama utekelezaji wa sheria hii unakuwa mgumu kwa sababu hatuko wakweli. Hivi ikiwa tunafuata kweli utawala wa sheria na ikiwa sheria zetu tunazifuata tulitunga

sheria zikaletwa Baraza hili hili la Wawakilishi, Sheria inayohusiana na mambo ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi tulitaka kila mwananchi atimize masharti ya sheria akishatimiza masharti ana haki kila mtu apewe haki yake kwa sababu ameshatimiza masharti.

Leo sheria hii ya maadili inakuja lakini pamoja na kuwa sheria ya maadili ni kwamba anatakiwa yule kiongozi awe mkweli, awe muaminifu, asibague, asibughudhi kuna vifungu humu vimeandikwa humu, kama asibague na asiwe muongo.

Mheshimiwa leo inasikitisha sheria tumezitunga kama mtu awe na cheti cha kuzaliwa akishakuwa na cheti cha kuzaliwa anapewa kitambulisho chake kwa sababu katimiza masharti, leo kuna watu wametimiza masharti yote leo tuna mwezi wa kumi na moja kuna watu wana miezi kumi na moja washatimiza masharti yote washapiga picha, washafanya kila kitu hawapewi vitambulisho wanazuiliwa hivi hivi, leo tunakuja na sheria hii ya maadili ya viongozi, hayo maadili ya viongozi na tumeshasema asiwe muongo, asibague, kwa nini wazuiliwe watu haki zao?

Leo mnasema sheria hii tuipitishe, tutaitipitishe hii lakini utekelezaji wake hautekeleze, mwezi wa sita huu watu wamezuiliwa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi wameshapiga picha, washafanya kila kitu wakifika wanapigwa danadana wanaambiwa mwezi huu mashine imeharibika, *material* ni mbovu, picha hazifanyi kazi, almuradi watu wanapigwa danadana tu kwa makusudi, ni ubaguzi na kuvunja maadili kwa sababu watu wana sheria zao. Washatimiza masharti kwa nini abaguliwe mtu asipewe? Waheshimiwa kusema kweli hizi sheria tunazitunga lakini hatuzitekelezi, tunazitunga wenyewe sheria zetu.

Leo tunasema kwamba mtu akisema uongo kwenye sheria za maadili kashavunja maadili, akibagua watu kashavunja maadili, kwa nini wanabaguliwa watu hivi sasa na nyote mupo viongozi mnayaona, lakini hili mumelinyamazia kimya.

Mimi binafsi nina mtoto wangu mwezi wa saba huu anapigwa danadana tu; kashapigwa picha, kashafanya kila kitu ametimiza masharti yote anapigwa danadana tu, akifika anaambiwa *material* mbovu, mashine ni mbovu kwa nini mnatufanyia hivi halafu mnasema mnatunga sheria ati mna maadili? Si kweli, hamna maadili, haya maadili ya viongozi hayataki kutekelezwa hilo ni jengine.

Leo watu wanapewa masharti mazito ya kubaguliwa kuwa wasipate, na sheria inasema isibague nataka nisome hiki kifungu, Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 66 kwenye jadweli la kwanza wanasema hivi.

Ukurasa wa 66 unasema;

"Kuhusiana na viwango vya maadili; kwamba viongozi watafanya kazi kwa uaminifu, ukarimu, umakini, kutosheka na kukuza maadili kwa kiwango cha hali ya juu imani ya wananchi katika utekelezaji wa Serikali bila ya upendeleo".

Sasa kama bila ya upendeleo kwa nini wanapendeleta wengine, wakifika saa ile ile wanapewa vitambulisho, akifika mtu akijulikana ni fulani saa ile ile anapewa. Tulipanga hapa na Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mwinyihaji Makame katika bajeti zilizopita, tukakaa kitako tukaenda majimboni tukakaa na watendaji tukazungumza nao, leo ukifika watendaji saa hizi wanakwambia mashine ni mbovu, hivi mashine hiyo inakuwa mbovu miaka yote lakini wengine kwa nini inakuwa ni nzima jamaa zanguni? Hivi tunaelekezana wapi jamani, huku kuna kukuza Serikali ya umoja wa kitaifa, huo umoja wa kitaifa utakuzika wapi kwa ubaguzi kama hivi, jamaa zanguni tusifanye hivi, na hizi sheria tukishazitunga tuzitekelezeni, unajua kama sheria imeshatungwa mtu asipotekeleza ile sheria ameshavunja maadili.

Sasa mimi nataka niambiwe kama hao wanavunja sheria ya maadili wanachukuliwa hatua gani, kwanza hiyo Tume itakayoundwa tunataku kuunda tume gani iwe ya uadilifu wa kutenda haki kweli tume gani itakayoundwa hata itekeleze hiyo haki, kwa sababu tume tunaziunda tukisha hatuziachii zifanye wajibu wake, hao watu wa vitambulisho hatuwaachii wafanye kazi zao tunawaingilia kati, sisi viongozi wa kisiasa tunawaingilia kati. Halafu humu tunatunga tumetia viongozi watupu ati tutekeleze maadili, hatutekelezi si kweli hatuitekelezi, hatutekelezi maadili Waheshimiwa tusemeni ukweli, tuweni wakweli, tuweni waaminifu, tunasema tusibaguane lakini tunasema kwa ncha ya ulimi tu kwenye nafsi haipo.

Waheshimiwa sheria hii nasema tena ni nzuri kweli kweli lakini haitekelezwi, hiyo Tume itakayoundwa hiyo watu hawataki ifanye kazi yake, itaundwa tume ikishaundwa tume tayari tutaingilia kati viongozi tuwapangie tusiwaache watekeleze kazi zao.

Hizo Mahakama hatuziachi zikafanya wajibu wake ingawa ni muhimili unaojitosheleza lakini hatuwaachi, kwa nini tunavunja haki za binaadamu, tunavunja sheria sisi viongozi kuna sababu gani kama sisi ni waadilifu kweli na tunatekeleza haki za binaadamu, wale Mashekhe wakachukuliwa na viongozi wengine wakasema muna viongozi wanasema tutawatia adabu kama tulivyowatia adabu mashekhe ikisha mnatunga sheria ya maadili humu mnakuja nayo tuijishe humu. Kuna viongozi wanasema nyinyi tutawatia adabu kama tunavyowatia adabu mashekhe, kumbe wale Mashekhe wanatiwa adabu si kwa sababu wana makosa, wanatiwa adabu bwana, leo mtu anasimama anasema tutakutia adabu kama tunavyowatia adabu mashekhe, jamani ikisha tunasema maadili, tuna maadili ya viongozi, jamaa zangu tunavyokwenda hii tunaitunga lakini haitatekelezwa hii jamani. Mimi sitaki niseme sana kwa sababu mengine nitakuja kulia humu na sitaki nilie.

Kwa hivyo naomba nimalizie kama nilivyosema hii sheria mimi nimeisoma sana ni Mjumbe wa Kamati, na hii sheria jambo ambalo nataka nimalizie, hivyo kama tutaitipishwa hii sheria basi Serikali ijjipinde kuipa Tume hii bajeti kubwa, kwa sababu bajeti utekelezaji wa tume hii ni uangaliaji wa mali za viongozi humu mna watu wana mali Kenya, Dubai, Mtwara, Mwanza; ufuatiliaji wake ni wa fedha, tumekwenda Dar es Salaam kujifunza kwenye Tume ya Maadili, wametueleza wao hivi sasa wana mshauri muelekezi hivi sasa wana mzungu anawaelekeza kwa sababu wao wameshindwa kuitekeleza inawabana mpaka utekelezaji ni mgumu. Imebidi kwenda kuchukua mzungu wanamlipa mapesa ili awasadie na awaelekeze, kwa hivyo na sisi kama tumeshajipanga kweli sio sheria tumeshaitipishwa itupwe ndani ya boksi hii itekelezwe, tunapitisha kamati humu kuna kamati ngapi zinaundwa humu za Baraza la Wawakilishi zimekuja na ripoti nzuri kweli kweli Serikali imeshindwa kuzitekeleza, hawajatekeleza hata neno moja.

Leo tunakuja na hii basi hii ikishapitishwa isitupwe boksini, itekelezwe kweli sisi tupo tayari tutaandika mali zetu na nyinyi muandike mali zenu, lakini mukishaandika hizo mali zenu tujue na sababu za mali zinazotoka lakini na wananchi jamani kama tunatunga sheria ya maadili tuwapeni haki zao, tukuze ule umoja wetu tunaosema tuiseme kwa midomo tusemeni kwa imani ya roho.

Jamani tunatoka dunia hii ni njia, dunia jamani ni njia, dhalma ndogo unayomdhulumu mtu itakwenda kudhuru, tusione mchezo tukaona humu duniani hivi sasa, jamani tatarudi kwa Mungu ameondoka huyu mwenzetu Issa huyu amekwenda kule ni mzima. Amekwenda kucheki afya kufika ye ye anaambwa huna kiungo hata kimoja kilichokuwa kizima saa ile ile alianguka.

Jamani na sisi tusecheze na dunia ni mapitio ya njia, unapomdhulumu mwenzako usione kama hatalipwa, jamani tutalipwa sote na kila mmoja atalipwa kwa makosa yake anayoyafanya, tusiadhulumu watu haki zao kuwazuia watu, ile haki unayoiweka ile sheria Serikali ni baba ya wananchi wake wote, sasa inapotunga Sheria yake kwa mwananchi na mwananchi akatekeleza ile sheria hiyo utamdhulumu washawadhulumu. Kwa nini tunatunga Sheria halafu hatuzitekelezi jamani.

Kwa hivyo, hii Sheria ni nzuri tuijishe ni lakini utekelezaji na Serikali nayo itekeleze wajibu wake. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana. (*Makofit*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mheshimiwa Subeit mchangiaji anayefuata ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, hakuna majina mengine yaliyofika kwa hivyo atakuwa mchangiaji wa mwisho kwa wale wanaotaka kuchangia walete majina yao.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wanaogopa hao kila Mheshimiwa aliyeokuwa hataki kuchangia ujue anaogopa pengine inawagusa na wao hiyo sheria.

Mhe. Mwenyekiti mimi leo sitokuwa mkali na kwa sababu sitokuwa mkali Mheshimiwa watu hii hawajaiona hii sheria, tunatitimka tunajikaza lakini ukinyoosha vidole vingine vinakuelekea nataka niwe taratibu sana Mhe. Mwenyekiti leo.

Sheria hii Mheshimiwa mimi naiogopa na kwa nini nikasema naiogopa Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo tunapitisha sheria ambayo tunawasaidia wanyonge, hii sheria hii ni ya wanyonge kuwatetea maana yake ukweli tuseme, kwa sababu tunaodhulamu ni sisi, tusione tabu kusema, tunaodhulumi ni sisi viongozi tunaharibu kutia mikono kusaidia jambo ambalo halistahiki ni sisi viongozi, na hilo tuliseme tusiogope.

Mhe. Mwenyekiti,, nina sheria kubwa sana ya mwaka 1995 Sheria ya Maadili ya Viongozi wa umma namba 13 wenzetu walitangulia kutunga sheria na utekelezaji wao ukawa ni mgumu sana katika kufanikisha au kutangaza kupeleka watu Mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, tuliunda kamati teule nyingi hapa na kamati zile za kitaalamu wakiwemo Wawakilishi wakapembua, wakaeleza sasa leo je sheria hii itaangalia katika zile kamati teule, au sheria hii zile zilizopita ina maana kwa Mhe. Waziri zitakuwa zimepita, hebu nipe vitu ukija hapa Mheshimiwa Waziri wangu kwanza hilo nataka nikusaidie kazi Mheshimiwa Waziri leo.

Mhe. Mwenyekiti, watu hawajafahamu nini maana ya umma, watu hawajafahamu nini maana ya maadili. Nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara hii na Naibu wake na Waziri wake na Wanasheria niwasifu sana wametengeneza msumeno wa ile kaset hawakutengeneza msumeno wa *power*, msumeno wa *electricity* wa *technology* ya kisasa unakata tu shaa, sio ule wa kwereche kwereche Mheshimiwa ile nakuwa tabu.

Mhe. Mwenyekiti, hata na mimi mwanzo nilikuwa nasema isije isije lakini leo nilifika pahali na mzee wangu Mheshimiwa Ali Mzee tukasema acha ije. Mheshimiwa Mwenyekiti imekuja hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikisema sana kwenye Baraza hili na watu huko nje mashahidi wanashuhudia nilijitolea rasmi kuwatetea wanyonge, haidhuru sheria ndogo ndogo zipo za mtu anayedhulumiwa, hata kwenye Katiba ipo wazi lakini utendaji wake ulikuwa sio kabisa kusema ukweli haki lillahi taala. Lakini kwa kuwa leo sheria hii imeanza kupita kwa Makatibu Wakuu ikapita kwenye Baraza la Mapinduzi, sasa imekuja hapa kuja kutungwa sheria.

Mhe. Mwenyekiti mtaalamu wangu tangu juzi nataka kukwambia hiyo siyo siri tumeshakaa vikao viwili vitatu mimi na Mzee Ali kuhusu sheria hii yuko wapi, yupo hapa Mzee Ali tumeshakaa mara tatu tumeshatafuta kila aina ya kitabu, ye ye katafuta kitabu tangu enzi za Karume, Jumbe zote tumetafuta tumekaa na kuweza kuona hali halisi ilivyo tukasema basi acha ije ili tuokoe wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Wizara hii alipanga sheria hii na kuiona hali halisi ilivyojitekeza kwa Zanzibar, wengi wamechangia sasa naomba Mheshimiwa niendelee katika kurasa ambazo nimeziona ili kuweza kuweka sawa kulingana na Mswada huo. Mheshimiwa watu watakuja kununa lakini wasinune, kwa sababu ndio moja katika kuweka mambo sawa. Sijui nani wananchi wamewaambia kwamba leo utakuja Mswada wa Maadili, simu yangu imejaa *messages* kibao. Kuna mmoja amenambia Mheshimiwa inashangaza sana mtu leo anafanya kazi ana jumba la ghorofa, utasema kama Sultani wa Saudi Arabia. Sasa Mheshimiwa zinafanya nini Sheria hizo, huyo namwambia kazi yake nimeshaifanya hii, na msahafu hautonikuta tena kwa sababu tumeapa hapa, namwambia kama yupo kwenye televisheni atasikia mwenyewe.

Namwambia kuwa sheria hii sasa ndio tunaitunga. Hao waliokuwa wanajilimbikizia mimali Sheria hii inasema kwa sababu kunatakiwa utaratibu, kila mtu. Maana sheria hii kila ikitiwa saini ikiwa sisi tutaingia au hatutoingia, watu wataanza wale maafisa. Maana yake sasa hivi tumo katika yaamu shaka, tupo *ICU* kwa maana yake niseme tuko *ICU* kuwa wakati wowote unaweza kuwa umekuwa hai, kwa sababu tupo katika kinyang'anyiro cha kutaka kupata jimbo. Kwa hiyo sidhani kama hii itatukuta, kwanza tukiingia sasa ndio itatukuta sheria hii. Sasa wale Maafisa waliokuwa wana miaka 60 katika kuendelea uhai wao wamo kwenye kazi sasa ngoma ndiyo hii hapo.

Mheshimiwa tuwe *serious*. Namuomba sana Mhe. Rais tuwe *serious* kwa sheria hii. Kwa sababu nchi yetu hii nchi ya Zanzibar tuseme ukweli sio nchi masikini. Na kama Sheria hii itafanya kazi mtakuja kunambia hata kama nikifa kaburini njooni mnitilie fat-ha mnisemeze pale. Tuone kama nchi hii tukiitekeleza Sheria hii kikweli kweli ipasavyo *wallahi* nchi hii hatutofanya bajeti ikawa pungufu kwenye matrilioni huko. Kwa sababu matrilioni yako nje, wanatumia watu na ndio maana ikadhamiriwa ije, hawa wanafanya dhamiri ya kuja hapa Mwenyezi Mungu awajaalie awape la kheri, kwa sababu wanawatakia kheri wananchi. Sio kitu cha mchezo mtu ana kijiji kizima, maulize kapata wapi pesa, hana historia ya utajiri, kama mimi utasema ok, labda Mshimba ana historia ya utajiri

kwa sababu baba yangu alikuwa akifuga ng'ombe wengi utaniuliza nini, ninayo historia ya kuwa na fedha, lakini mtu anaingia ana miaka mitatu miaka minne yupo kazini na ndio maana wenzangu wanasema kweli mpo *serious* na Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, *wallahi* sikufichi zile fedha zao ambazo tutakapokuwa mtu, kwa sababu wengine wanashindwa, hatuwezi kusema kwamba mimi nina nyumba moja si kweli, tuna udanganyifu tunaandika jina la Mwajuma lakini wataandika ile nyumba ili wasijue, si mchezo. Ndio maana nikasema sheria hii wanaohusika Tume itakayoundwa iende *deep* kweli si kitu cha mchezo. Lakini watu wengine hawajui kumbe Mwanajuma wenyeve kaandikwa sasa hivi hata ile kazi ya Manispali hana, ukioneshwa hiyo nyumba yake ni kubwa sana, wee huzimii. Maana yake vitu vyengine vya kuogopesha sana.

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe tunakuwa viongozi tunaingia katika mambo ambayo hayahusiki, ni makubwa tunatia mikono ovyo ovyo. Kwa kweli mimi hili suala linanitisha sana, lakini mimi nataka niseme kitu kimoja. Nina ushahidi wala sisemi kwa kubahatisha, kaka yangu hapa mmoja aliymaliza alizungumzia suala la vitambulisho. Nina ushahidi na mpaka leo watu wameandika vitambulisho hawajachukua, nimekwenda kuviona mimi mwenyeve. Je, sheria hii itawakamata?

Sasa haya mambo ndio nikasema tuyaaangalie, tunavyofanya hili suala maana hii Sheria inacheza, ina *hang*. Mheshimiwa kasema sana hapa, maana lazima tulielewe hili suala kwa mujibu wa Sheria ya Maadili yenyeve yakoje yanayotakiwa ya kiongozi ayapate, tusiingilie katika Ofisi zetu. Mahakama iende kwa mujibu wa sheria zao, Mahakama iamue kwa mujibu wa sheria zinavyowapa. Halikadhalika na masuala mengine yaendelee vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi najiuliza swali moja, lakini kwamba namuomba Mhe. Rais asichelewe kuitia saini, namuomba sana. Mhe. Rais, leo tukimaliza asubuhi jioni mwaga saini, kabisa, si mchezo, hii isichelewe Mheshimiwa. Kwa nini nikasema Mhe. Rais asichelewe, kwa sababu watu watafanya haraka haraka haya mambo watu waibe, watu watanyang'anya, watu watawadhulumu watu, watu watakwenda kusimamia mikataba mibovu, tunaletewa haraka haraka kwa hivyo Rais akichelewa watachukua nafasi hii hapa, asiwape *gape*. Tunamuomba sana Mhe. Shein unikisikiliza kwa shingo upande kabisa, hichi kitu kimeanzia kwako kimekuja kwetu sisi na wewe ukija tu Mheshimiwa amwage saini aweke historia katika mswada ambaa atakaoutia saini mapema huu. Ndio Mheshimiwa hatari hii.

Mimi nashangaa siku zote tukija hapa Waziri wa Fedha anatwambia uchumi umekuwa, na ni kweli uchumi umekuwa, uchumi umekuwa Mshimba ana gari tano, wapi kapata *I don't know where*, siwezi kujua. Sasa hii sheria utataja, maana yake uzuri wa sheria hii usijinyime mwenyeve ukajikuta unaingia katika sheria, bora ujitate useme nina gari tatu kuliko kuja kusema una gari mbili kumbe una gari tatu. Ukitsema una nyumba kumi, bora ujieleze kwani si aibu, si tena utatizamwa hizi nyumba ulizipata vipi. Ndio maana ya sheria hii. Kwa hivyo naomba Mheshimiwa hili suala Mheshimiwa asiliweke *pending*, atutilie saini.

Mhe. Mwenyekiti, wanasheria walijitahidi sana, Wizara imejitahidi sana, Kamati nayo imejitahidi sana. Lakini pamoja na Mwenyekiti wetu kusema kuwa kwa sababu Mheshimiwa hili suala kusema la ukweli tumejaribu kwenda na wenzetu Bara. Wenzetu Bara wametwambia sheria yao na wametwambia hasa hili ni suala gumu sana, hata hivyo walijitahidi waliweka zile *branch* mimi natoa *suggestion* na mimi nasema kuwa Sheria hii itakapopita tuanzie katika Shehia, kuwepo Wajumbe *and then* labda Wilaya na Mkoaa hapo Mheshimiwa utaweza kufanya kazi vizuri, kwa sababu kwa kungojea wewe Tume iletewe tu, mawe! Tunajuana Zanzibar hapa unafanya mchezo utampatia mtu atakuja wapi haji, lakini ipeleke kule kwa wananchi ianzie sheria kwa wananchi, ukianzia sheria kwa wananchi Mheshimiwa utafanikiwa kwa sababu mwananchi ana uchungu na kodi yake anayolipa.

Ndio maana Zanzibar kusema ukweli suala la kodi wananchi hawajui na hawajajua hasa ile faida ya kodi, hawajajua ile kodi yao wanayolipa na ndio maana Zanzibar kusema la ukweli suala la kodi hawajui hasa ile faida ya kodi. Watu chungumzima kodi wanakimbia, matajiri wakubwa wakubwa kodi wanazivunja hawazipeleki, Sheria hii itawafunga sasa hivi.

Hao waliokuwa hawataki kulipa kodi watu wakubwa wakubwa kama wamo humu Baraza la Wawakilishi siwataji, matajiri wakubwa wakubwa kama hawalipi kodi hii, Sheria itawafunga hii. Hii Sheria kifagio haichagui mtu. Wananchi watajua sasa faida ya kodi yao. Hili tuliseme tusiliogope, kwa sababu ukiogopa kusema huwi kiongozi mzuri, lazima ukweli useme.

Mhe. Mwenyekiti, leo madawa hakuna, lakini ukiangalia fedha zinakwenda wapi na kila leo mizigo inashushwa, tunawachangisha wananchi kulipa kwenye madawa haya, kwenye mahospitali na kila kitu, kutokana na kutokuwa na fedha za kutosheleza za kuwanunulia dawa hospitalini. Kila siku hospitali ile pale, si kama natania hapa nikisema jina la rufaa liondoshwe, rufaa sio jina la Mwakilishi, lakini nikaambiwa hapana tusiiondoshe na mimi nikaikubali. Lakini wanakwenda tata, wanajitahidi kutokana na hali halisi ilivyo. Na bado hawajafikia kwa sababu hawana, bajeti yao ni ndogo zinaishia mikononi, bajeti ndogo zinaishia mifukoni.

Naomba sana sasa lishughulikiwe hilo.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja Mhe. Waziri alikamata watu kibao kule Bandarini, Mwenyezi Mungu amjaalie ajitahidi hivyo hivyo, Nalionna alivyookoa zile fedha ziliviyokamatwa. Sasa sheria hii Mheshimiwa tuisiwabughudhi. Tena mimi naomba sana kama ikiwa tunakusudia hii Tume watakaofanya kazi watoke kwenye maidara, tumeimaliza, tumeiangamiza, watoke nje, wapo vijana wetu watoto tena nakwambia kweli, niko *serious* tusifanye kama ile Takukuru ya Zanzibar tulichagua tukawachukua watu ndani ya mawizara tunakosea hapo Mheshimiwa. Kamchukue mtu huyu chini, waliomaliza kidatu cha nne wapo kidatu cha sita wapo, hajaonja utamu huyu, kamchukue huyu. Halafu m-*train* na ku-*train* yenyewe sio unamuweka hapa hapa, mtoe nje kidogo afahamu hiyo kazi yake aijue, kampike nje.

Hii Tume isifanye ubahili, toa watu nje, wapeleke watu wakasome vizuri, anzia sasa, hii itapita ushapita isiwe na wasi wasi kelele za Waheshimiwa hatuzijali ishapita, kula suti tu Mhe. Waziri hii ishapita usiwe na wasi wasi. Lakini tuangalie watu gani wa kuwaweka pale. Ni watu ambaeo wa kuwachukua kutoka majimboni ambaeo watu bado wanaona huo ukali wa maisha, Wallahi watafanya kazi Mheshimiwa. Hiyo natoa rai yangu naomba sana hilo. Hilo naliomba na ndio nime-study sana hizi kama tunavyoziunda. Kamati tunazoiunda tunatoa watu mle mle kwenye *department*, haifanyiki vizuri. Sasa hebu itoe hii itengeneze upya uone, katibu kachukue watu huko nje majimboni na si vibaya wakenda wakachukua Jimbo la Kitope wapo kibao kidatu cha sita. Ndiyo, kwa nini nimtetee mwenzangu nasema kwangu, wapo vijana kule vijiweni, wanaolia na ukame huu, leo watizame wale watoto wanavyoji-*train* uone kama hukufanya kazi vizuri. Watasema tu, Mshimba ana gari kumi. Wallahi atakwambia kwa sababu hapo nimemleta mwenyewe ataficha siri hapo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sheria hii irudi chini kwa wananchi ndio wawe wateule ili kuwapeleka juu, na mimi najua hili jambo Mhe. Waziri ukikaa na Rais najua hili suala litapita tu, sasa uone hapo kazi hii itakavyofanyika. Sasa hivi tuna Kamati Teule Moja ya kufuatalia suala lile la nyaraka.

Mheshimiwa Kamati nawaambia kuwa wa *delay* hivi hivi ipate kutiwa saini Kamati, pale manyaraka kibao yamepotea hapa, kwa hivyo tusiogope Mheshimiwa. Wa- *delay* hivi hivi Kamati waende taratibu taratibu ndio tunapoanza hapa na nyinyi hapa ndio mtaposifiwa Wajumbe wa Kamati Teule, kwa sababu tayari pale pataonesha dhahiri kuwa kweli hii sheria tunayoifanya kazi na wakati huku tuna kamati teule tumeshaanzishwa kuiunda hapa. Tizama sasa mchezo unavyokuwa, kwa sababu pale kweli ubadhirifu upo na watu wanajua wengine wameshaona. Kwa hiyo sasa tuendane na hii sheria inavyokwenda kwa utaratibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe wazo langu jengine. Mimi napenda kutoa ushauri wangu bure wala sio *expert* wala sipati kupewa pesa na kila kitu. Kwanza unapoanzisha vitu kama hivi inavyotakiwa tuwe na mambo ya teknolojia; *information* za teknojia kwanza tuwe nalo hilo, pili tuwe na *transport* ambayo itakayoweza ku-*play* kila sehemu ya Zanzibar yetu. Lakini tatu Ofisi yake iwe *independent* na Ofisi ile ya aina nyengine isiji-*include* na Ofisi nyengine, tukaizalisha ndani ya Ofisi tukasema Ofisi ya Rais Ikulu tunaiweka hiyo. Itakuwa tumeipotosha. Mimi naomba hilo Mheshimiwa hili suala uweze kulikubali kwa sababu ni suala ambalo *simple*, kwa kutokuwa na *information* ambazo zinakwenda na wakati ni kupoteza taarifa ambazo wale wachunguzi wamekwenda kuleta pale, naomba tuanze mapema kwa sababu kama nilivyokwambia hili Mheshimiwa ataitia saini sana.

Mheshimiwa nimalizie, kwa kumaliza kwangu viongozi wenzangu, Mawaziri, Waheshimiwa, Makamo wa Pili, Makamo wa Kwanza (*Makofi*)

Mnapiga makofi hamjui ninasema nini, nimesema wote wametajwa humu kwenye sheria hii na mimi nimo sijakataa. Nimesoma sote tuliotajwa humu kwa hiyo naomba sana ili nchi yetu ipate iende vizuri, ili nchi yetu iwe na maadili mazuri ya umma; sheria, sheria, sheria, isitiwe mkono, tukae huko pemberi. Jamani kwani ukisema kwamba hapa nilipofika basi kuna tatizo gani. Kama huko nyuma ulidhulumu, watu wanakwenda Makka hapa kujisafisha, eeh

wanasema kwamba sasa hivi nakwenda Makka kujisafisha, basi, yalipofika basi. Na sisi tufike pahali tuseme tunaona Sheria hii, kila Mjumbe humu ajijue kuwa tunasema basi, tulipodhulumu, tuliponyang'anya tunasema basi kwa sheria hii isitukamate.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na nampongeza sana Mhe. Waziri, nampongeza sana Katibu na Naibu Katibu na Wakurugenzi wake, *Inshallah* kheri na mimi Sharifu naitilia baraka na naiunga mkono kwa asilimia mia. Ahsante sana.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi pia kunipatia fursa hii ya kuweza kusema machache sana. Kwa sababu huu Mswada ulituhangaisha sana sisi. Mpaka jana tulikuwa nao tunatafuta roho pa kuitia, halafu tukafika saa nne za usiku, leo tumeshindwa kuwasilisha taarifa asubuhi kutokana na haraka ya mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa kunipatia fursa hii. Awali ya yote nichukue fursa hii kutoa pole kwa Mwenyekiti wa Chama changu Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, pamoja na wafuasi wenzangu wa Chama cha Wananchi CUF kwa kuweza kupata kisago cha serikali pale Kariakoo. Mimi nadhani sasa tunaanza kupasha, katika hili natoa pole sana na namuomba Profesa na wanachama wenzangu wasivunjike moyo, kwa sababu *working hard is a source of success*, naamini tu kuna siku tutafanikiwa tu *biidhnillaahi*.

Baada ya hayo sasa niende moja kwa moja katika Mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu kwa kweli mimi unanipa shaka sana. Kamati yetu sisi tulilazimika kwenda Dar-es-Salaam kwenye Tume ya Maadili, tukaenda Dodoma tukazifua Kamati hizi zinazohusiana na mambo haya pamoja na Katiba na Sheria. Tukapata mafunzo mengi sana kama alivyoleza Mwenyekiti wa Kamati hapo awali. Tulisema kwamba tungepewa muda wa wadau wa haki za binaadamu na wataalamu wengi ili kukaa na serikali wakashauri na ile Kamati kupata nafasi ya kwenda katika nchi kadhaa ambazo nazo zimeanzisha sheria hii. Lakini hadi sasa utekelezaji wake nchi hizo zimeshindwa kutekeleza. Tukaambiwa Ghana wametunga tukaambiwa hadi leo haina utekelezaji. Tulitaka kwenda kujifunza kidogo pale Ghana kwamba kwa nini wameshindwa ili na sisi tuje tulete uzoefu, lakini na Ofisi ya Spika, nadhani mambo si sawiya katika mambo ya madukhuli tumeshindwa.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kwamba sisi kazi zetu ni kutunga sheria tu. Ama sheria maana Mhe. Subeit alisema kwa kutunga sheria nzuri. Mimi napingana naye sio kwa kutunga sheria nzuri bali ni kutunga masharia mengi tu, lakini sasa utekelezaji wake unakuwa tatizo. Hivi sasa tumeanzisha yaani tumeshatunga ile Sheria ya mambo ya rushwa ile ipo, lakini Mheshimiwa inasikitisha sana kwamba sheria ile ipo lakini utekelezaji wake unakuwa tatizo, mtu anakuwa anaingia katika Taasisi siku mbili tatu analala katika kibanda cha tende yaani vibanda vile vya kawaida lakini baada ya miezi michache unamkutia analala katika makasri mawili matatu manne na sheria ipo, lakini sasa tunaleta na sheria hii Mheshimiwa. Mimi nadhani Mheshimiwa katika hili uniache kwanza msimamo wangu uko mbele niingie sasa katika huo mswada.

Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia hapa ukurasa wa 56 wa huu mswada kifungu cha nne kinasema kuanzishwa kwa Tume ya Maadili ya viongozi wa Umma, naomba ninukuu kidogo Mheshimiwa.

"Inaanzishwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ambayo itakuwa ni Wakala wa Serikali".

Naomba hii Wakala wa Serikali niinakshi *with capital letter* Wakala wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa Serikali yenye kwa kipindi chote hiki imeshindwa kusimamia maadili katika nchi hii itakuwa wakala wake, mimi nadhani hili tatizo lipo na kuna haja sasa Serikali kuinama ikiwa mama kashindwa mtoto je? Maana Mheshimiwa tuna *experience* nydingi zinazofanywa *ku-doubt* habari ya hii Tume, Mheshimiwa tuangalie pamoja na maadili ya nchi ni pamoja na kusimamia haki za binaadamu, ni pamoja na kusimamia Katiba ya Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tuangalie Katiba ya Zanzibar katika ukurasa wa 7 kifungu cha 11(1) inazungumzia usawa wa binaadamu. Naomba niinukuu hii Katiba.

"Binaadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa".

Sasa kusimamia Katiba ni mionganoni mwa maadili ya viongozi, lakini Mheshimiwa inaonekana kwamba Serikali imekuwa *bias*, *it has got double standards*, ina *double standard* baina ya raia wake, ikiwa leo Serikali ina *double*

*standard* tuna mtoto wake je, huyu wakala ambayo ni Tume ya Maadili atawenza kweli. Mtoto siku zote hufuata kichogo cha mzazi wake, na hili sasa Mheshimiwa naona *waste of public funds*, kukaa hapa sisi tukatunga kitu ambacho Serikali yenye imeshindwa kusimamia, leo tunaleta Tume ambayo ni wakala, Serikali imeshindwa kusimamia Katiba yake katika usawa wa binaadamu ninayo mifano Mheshimiwa, ninayo mifano mingi tu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni kuna Kasisi mmoja alimwagiwa tindi kali walifika hapa mpaka FBI kuja kufanya *thorough study* ya kwa nini Kasisi huyu akamwagiwa tindi kali. Kwa kweli hivi juzi katika Mahkama walikuja masheikh wakasema wanadhalilishwa kijinsia, hatujapata taarifa ya Serikali yoyote, hatutaki kuja FBI kuja kuwasikiliza wale masheikh mule ndani lakini Serikali hajatoa tamko hajakubali wala kukataa kwamba maneno waliosema kina Sheikh Msellel mule wana hili, neno ni zito mimi nadhani nisiliseme ninyamaze. Wanadhalilishwa kijinsia, sasa katika hili Serikali hata tamko basi hamuoni kama hiyo ni idhilali, hamuoni kama hiyo ni *double standard*?

Leo ikiwa Serikali mumeshindwa kusimamia Katiba ya nchi na ule usawa wa binaadamu kwa mujibu wa hii Ibara ya Katiba tulioitunga, leo mnataka kuanzisha Tume ije, itakuja kufanya nini hapa si itakuwa inafuata kichogo cha mzazi wake tu.

Jengine Mheshimiwa nimeangalia Katiba vile vile Ibara ya 6 (1) inazungumzia suala la mzanzibari.

"Kutakuwa na Mzanzibari ambaye upatikanaji wake na urudishwaji wake utakuwa kama ilivyoainishwa katika sheria iliyoitungwa na Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Spika, kuna hii *Zan ID* ambayo ni haki ya kila Mzanzibari hivi sas Serikali ambayo hawajaleta hiyo Tume ya Maadili Serikali yenye mpaka sasa upatikanaji wa *Zan ID* kwa wananchi ni tatizo sana. Sasa leo munaleta hii sheria tuipitishe hapa tushakaa siku nzima tushalipwa posho na Serikali hapa siku hii ya leo tunatunga sheria hii lakini Serikali yenye imeshindwa itakuwa Tume kulikuwa kuna haja ya kuileta hii, si bora mungeendelea *ku-violate human rights* na kufanya *double standards*, Mungu tu ndiye mkubwa!

Mhe. Mwenyekiti, mimi naitahadharidha sana Serikali katika hili suala nilolizungumza mwanzo la masheikh nataka *ni-declare interest*, mimi Mheshimiwa ni muislam na ni muislam lakini vile vile ni mwanasiasia. Lakini nataka mujuwe kama mimi ni muislamu zaidi kuliko mwanasiasia. Kwa hivyo, imani yangu ya kiislam naithamini zaidi kuliko siasa. Kwa hivyo, naweza nikaacha siasa lakini siwezi kuuacha uislamu.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa mtapitisha sheria hii na hii Tume ikapita ikaja hapa ina jukumu kubwa sana katika kutekeleza maadili ya nchi. Viongozi lazima hapa kama Tume itakuja ina kazi, kwa sababu Serikali imeshindwa, mimi naamini Mheshimiwa ikiwa Tume hii imekuja na mambo yakaja vile vile kwamba mtu anadhalilishwa, muislamu anadhalilishwa, hakuna Serikali inayoangalia, hakuna taarifa inayotolewa na Serikali, leo tunajiuliza sasa Serikali, naamini hatutapata jibu kuhusu wale masheikh wanavyodhalilishwa ndani, itafika pahala nilisema asubuhi kwamba waislamu watakuja kufika pahala wafuate maelekezo ya dini yao mta-*create chaos* katika nchi, mtavunja amani ya nchi. Mwenyezi Mungu kasema sote waislamu, kwa sababu waislamu tupo hapa, wapo Dar es Salaam, waislamu wapo Japan, waislamu wapo Cuba. Sasa wakija wakifuata maadili ya kwamba "*almuslim man salimal muslimina min lisaanihi wayadihi*" hamuoni patakuja ruka kivumbi hapa. Nadhani Serikali iwe makini sana.

Halkadhalika kuna watu wanapenda haki za binaadamu kwa mfano Waingereza, Wamarekani, wanapenda sana suala la haki za kibanaadamu *regardless* na *religious differences*, wao mnataka haki za binaadamu na kwa mujibu wa *The Holy Qur-an* inasema tumewaumbeni katika rangi na makabila tofauti ili mujuane tu.

Leo Serikali kwa kukiuka maadili kuwadharau wale masheikh mule ndani malalamiko yao wakija wakisema watu wa haki za binaadamu wanataka kuja kutetea binaadamu wenzao huku kupitia hiyo kauli niliyoitaja je, hapatakuja kuwa tatizo.

Mimi nadhani isisainiwe kwanza hii sheria kwa sababu munaweza mukaipitisha mimi siiungi mkono, munaweza mukaipitisha humu ndani lakini naomba sana Serikali kwanza *i-turn mindset* yake ya kuweka *balance* katika uendeshaji wa mambo ya Serikali, kuficha makovu walioyasababisha huku nyuma, kutoa haki kwa wananchi wote ndio baadae muulete tena.

Sasa kuna *turn mindset*, mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Serikali iurudishe huu mswada ikishaurudisha itafute wataalamu katika mambo ya haki za binaadamu na wanasheria wake nao, na sisi wataalamu katika mambo ya milahata na watu watuite tuje tutoe mawazo yetu ndio walete tena huu muswada, huu mswada haufai. Serikali yote nzima hatunzungumzii huyu wala huyu, kwa mfano hivyo vyeti nya kuzaliwa, vyeti nya kuzaliwa navyo kila mtu ana haki ya kuwa *registered* katika nchi. Na kwa bahati nzuri maana mimi niliyesimama hapa ninayechangia ni CUF na Wizara hii ina huyo huyo CUF lakini Serikali yote ni akhasi *regardless* kwamba Wizara anaongoza huyu au anaongoza huyu huu ni mkakati. Haya ilikuwaje nyinyi museme msiwabebe vyeti nya kuzaliwa CUF awabebe vyeti nya kuzaliwa na Waziri anatoka CUF.

Mimi nadhani ni tatizo hili Waheshimiwa ni Serikali nzima hili, ni Serikali nzima ni mkakati wa Serikali, lakini mimi ninachowaambia waheshimiwa lazima tukae pahala tuweke mambo sawa, juzi hapa wakati najibiwa hoja naambiwa kwamba nilisema hapa habari moja jana nachangia changia nilikuwa sipo nikasikia kupitia runinga tu kwamba aa mambo haya anayosema Mhe. Saleh hajui kuna watu watamchukulia hatua hapa. Mimi mwanangu hatua nishachukuliwa zamani sasa labda nichukuliwe guzo tu lakini hatua nishachukuliwa zamani mimi. Maana mimi nilioa siku ya Alkhamis, Ijumaa nikakamatwa nikawekwa jela, je kuna jengine kubwa kama hilo, mimi sasa hivi nasubiri kufa tu. Lakini Waheshimiwa ninachowaambia Serikali munatudhalilisha na kuna siku wananchi watachoka na wala hili si katika kutishana.

Mimi naamini nilivyokuwa nimeumbwa nitakufa vile vile, sasa kama mtu atakuja tia msaada wake ili nife anajitafutia jukumu tu, kwa sababu mimi kila siku nasema naishi kwa dawa. Sasa mtu akiija akitia nyalio unamuua.

Mimi nawaambieni Waheshimiwa kwamba toeni vitambulisho nya Mzanzibari Mkaazi, toeni vyeti nya kuzaliwa kinyume na hivi, waheshimiwa hii mnayofanya ni dhulma, hii mnayofanya ni *double standards*, wananchi na mimi nina ushahidi tosha kwamba Sheha wa Matale nilikwenda nao vijana 27 na kila mmoja ana *certified copy ya birth certificate* akawakimbia na hakuwatilia *sign* na kwenda kupata *Zan ID*, ni maelekezo kutoka Serikalini na badala yake akawachukua vijana wadogo wadogo *under age* waliwaandikisha *under age*.

Sasa kama nitachukuliwa hatua haya, lakini nasema kwamba ikiwa wamepewa wale *Zan ID* na kupewa *vote certificate* ili waje wapige kura watoto wadogo wale, natoa taarifa kupitia Baraza hili wasije karibia. Wasije karibia katika *polling station*, na ikiwa mzazi anamtaka mtoto wake asije mruhusu siku ile *under age* kukaribia *polling station*, kinyume na hivyo ni jino kwa jino. Ahsante sana.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu ambaao ugumu wake umeelezwa vizuri na Mwenyekiti wa Kamati aliyeuwasilisha hivi punde.

Kabla ya kuingia kwenye mswada huu na mimi niungane na Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kumpa pole sana Mwenyekiti wangu wa Chama Taifa kwa namna alivyodhalilishwa na Jeshi la Polisi. Lakini vile vile nilaani vikali sana matendo yaliyofanywa na Polisi jana katika kumdhulilisha Mwenyekiti huyu mtu na heshima zake, mtu anayefuata taratibu zote kama ambavyo imeonekana. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye mswada.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ukifungua ukurasa wa 56 kifungu cha 7(1)(b) sifa za Mwenyekiti. Mwenyekiti ana sifa zifuatazo:

Kwanza awe ni mazanzibari lakini pili mwenye sifa za kuwa Jaji wa Mahkama Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba hii ingefafanuliwa zaidi kwa sababu kama wenzangu ambavyo wamesema, masuala ya upendeleo wa namna mbali mbali yamekithiri hapa. Sasa ukianza kupendelea maana yake unaanza vile vile kumdhulumu mtu, sheria zinapindwapindwa, sheria zinabadilishwa sababu zinatolewa, lakini unajua kabisa kwamba huyu hana sifa hizi lakini amefanywa kuwa na sifa hizi.

Sasa hii ninafikiri ingefafanuliwa kabisa zionekane kabisa sifa ni hizi, suala la kwamba mwenye sifa za kuwa, hii bado haijakuwa *clear* na sidhani kwamba kwa sheria hii kwa sababu sheria hii kama alivyosema Mwenyekiti, sisi tu hapa tushahirisha kikao kwa sababu wenyeviti au kamati haijajiridhisha. Na kamati hii ambayo Mwenyekiti wake Mhe. Hamza ilioneckana kwamba ni ndogo kiasi ambacho wenyeviti wote wa Kamati zote ikawa sasa hivi na wao wameomba kusaidia.

Sasa unapopitisha sheria ambayo pamoja na ukubwa huo, na tuisahau haikuja hapa mpaka imepita kwenye Baraza la Mapinduzi, imepita kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu, kwa hivyo lazima tuwe na hadhari sana ili kuonekana kwamba hakuna jiwe ambalo halikugeuzwa. Kwa hivyo kuwa awe na sifa za kuwa Jaji wa Mahkama Kuu ingefafanuliwa vizuri.

Kifungu hicho hicho cha 7(3)(c) ni mtu aliyetiwa hatiani na Mahkama au chombo chengine chocchote cha kinidhamu kwa makosa ya uadilifu au uaminifu. Mimi nafikiri tungekwenda mbali zaidi, uadilifu uaminifu lakini kuna mambo mengine kama kiongozi vile vile hupaswi kuteuliwa kama una sifa au kama una aibu hiyo. Kuna makosa ya jinai ambayo unaweza kusema kwamba hili kosa la jinai hili kwa liliyofanyika na aliyelifanya ni huyu haiwezekani kabisa kabisa. Kwa hivyo nafikiri hapa tungeongeza kitu chengine kosa la jinai.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 58 kifungu cha 12(3) katika kufanya kazi za Tume chini ya sheria hii Mwenyekiti hatolazimika kufuata maelekezo au hatokuwa chini ya udhibiti wa mtu au mamlaka yoyote. Jamani hii *power*, ni *excessive*, hii nguvu aliyopewa Mwenyekiti ni zaidi.

Mhe. Rais katika Katiba imeelezwa kwamba anaweza akashauri lakini halazimiki kuchukua ushauri aliopewa lakini anashauriwa. Sasa huyu unaposema kwamba mimi najiuliza kwa nini hivyo Tume hii pamoja na ukubwa wake ina ukubwa wa mkubwa wake au kiongozi wake kupewa *power* hizi.

Sasa mimi nafikiri hapa hizi *power* mtu akishaona kwamba mimi ndio *top of the bar* anakuwa na kifuta, unamsababisha aringe si kwa uadilifu lakini kwa namna ambavyo yeye mwenyewe anahisi, kwa sababu hakuna mtu wa kumuelekeza vyengine yeye ni mwisho. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti ni vizuri kwamba hapa pafanyiwe marekebisho kidogo asipewe nguvu kiasi ambacho akajiona kwamba yeye ndio wa mwisho.

Ukurasa wa 60, kifungu cha 18 (i) mpaka (xi) hizi zinaleza kwa kuzingatia masharti ya sheria hii Kiongozi wa Umma atatakiwa kuzingatia miiko ya kijamii na kuepusha na tabia zifuatazo; zimetajwa pale moja, mbili, tatu, nne, tano. Lakini zote hizo rushwa haikutajwa hapa sioni, utoaji wa siri, uzembe, kushindwa kutunza familia, kushirikiana na watu wengine, kushindwa kulipa madeni, kutumia kauli ya lugha isiyofaa, ugomvi, unyanyasaji wa kijinsia lakini rushwa haipo, na rushwa ndio mwiba, msumari wa jahazi huu.

Kwa hivyo, na hapa iwekwe kwa sababu anaweza akala rushwa halafu akaonekana kwamba yeye hayumo katika jubilii hili kwamba hafai.

Mhe. Mwenyekiti, uvunjaji wa maadili kifungu cha 20 (a), (b), (c), (d) mpaka (i). Mheshimiwa mimi nashauri kiongezwe kifungu kingine “kauli chafu na zinazochocha chuki”.

Mhe. Subei Khamis Faki alisema hapa kwamba kwa Kiongozi wa Umma unapotoa kauli zinazochocha chuki ni hasara kubwa sana, yeye amesema kwamba kuna kiongozi ametoa kauli mbele ya hadhara kwamba tutakufanyeni kama tuliyowafanya watu fulani. Huku ni kujipa watu bure jamani pengine hata hayumo lakini jazba tu. Sasa hii inachochaea chuki, kauli kama hizi zinapotolewa baada ya mswada huu kupitishwa lakini kwamba *possible* huyu mtu hafai, huyo mtu hafai na hii itatujenga sisi sasa tuwe na hadhari katika kutoa hotuba zetu na jazba zetu.

Watu wanawenza kupigana kwa maneno tu ambayo pengine wewe ulipoyasema kwa jazba na baadaye ukaambiwa unajua umesema hivi, unajua umesema hivi unajilaumu mara mbili, nimesema na hivi. Sasa hii ukijua kwamba nikisema hivi litakalonipata ni hili na kuwa *disqualified* kama Kiongozi wa Umma. Mimi nafikiri sote tutakuwa na hadhari, tutapita katika mipaka.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 27 Tume kutoa maamuzi pale kuna 27 (1) na 27 (2), mimi niko kwenye 27 (2). Kwa masharti ya kifungu hiki Mwenyekiti atatangaza maamuzi ya Tume dhidi ya malalamiko au madai yaliyosikilizwa, dhidi maana yake ni (*against*). Sasa hili neno hili lioneolewe. Mimi nikisema nitatoa kauli dhidi ya Mwenyekiti maana yake ni kwamba kauli nitakayota ni kinyume na Mwenyekiti kauli yake au vitendo vyake.

Kwa hivyo, hili neno mimi nafikiri lingeondolewa hapa na likawekwa neno jengine, ingawa miswada hii kwa Kiingereza neno ni safi kabisa, lakini kwa Kiswahili hili litafutiwe neno jengine zuri zaidi ili liwekwe.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 41, ukurasa wa 65 Waziri anaweza kutunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa sheria hii, lakini 43 waziri ataweka. Sasa hapa mimi nasema kwa sheria hii ilivyo ngumu, ilivyo nzito tusimpe *option*,

tusimpe *free*, liwe kwamba anaweza, akitaka, asipotaka hafanyi, sasa kwa sheria hii ilivyo halazimishwi hasa. Kwa hivyo, Waziri atatunga kanuni sheria hii ni ngumu, si ngumu tu kwa kuisoma lakini ugumu wake vile vile katika kutekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 43 Waziri ataweka utaratibu utakaowezesha Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti, sasa sikuona popote katika mswada huu pengine na hata katika marekebisho ya kamati kwamba kuna nafasi ya Naibu Mwenyekiti. Sasa huyu hapa tu ndio alipotajwa kwa hivyo na yeze kama kuna Mwenyekiti na kuna Makamishna wengine wawili maana ndio Tume nzima hiyo, basi tuone Mwenyekiti amepewa sifa zake na huyu Naibu Mwenyekiti ni yupi, anapatikanaje.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakwenda ukurasa wa 66 jadweli la kwanza.

1. Maadili ya Viongozi wa Umma yatalenga kwa kadri iwezekanavyo kuweka na kukuza misingi ifuatayo kulingana na matendo ya viongozi.

(a) Kuhusiana na viwango vya maadili; kwamba viongozi watafanya kazi kwa uaminifu, ukarimu, umakini, kutosheka na kukuza maadili kwa kiwango cha juu ili imani ya wananchi katika utendaji wa serikali bila ya upendeleo uimarike.

Hapa mimi napendekeza kwa sababu huku nyuma siku zote uaminifu unakwenda na uadilifu, sasa hapa liongezwe neno jengine la uadilifu, uadilifu *is stronger* kuliko uaminifu.

Kwa hivyo, hapa nilikuwa nashauri kwamba tungeweza kuliweka hilo neno ili ukurasa 68 (5) unasema kwa hiyo, kila Kiongozi wa Umma niko kwenye (b) sasa aheshimu, asaidie na atekeleze maamuzi ya Mahakama maalum ikiwa ni pamoja na Mahakama maalum ya viongozi. Hii vile vile suaona kutajwa mahali Mahakama maalum ya viongozi, wala sijawahi kusikia mimi katika nchi hii kuna Mahakama ya Kadhi, Mahakama ya Ardhi, Mahakama Kuu, Mahakama ya Mkoa, Mahakama ya Wilaya, lakini Mahakama maalum ya viongozi iko wapi labda pengine waziri akija hapa wakati wa kufanya majumuisho atatwambia Mahakama Kuu ya Viongozi iko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, tabia haina dawa tangu Baraza hili lilipoanzishwa tumekuwa tunatunga sheria mbali mbali, kama ambavyo leo sasa hivi tuko hapa tunatunga sheria hii tunayoizungumza. Sheria zipo nyingi nzuri tatizo tulilonalo kwa miaka yote ni utekelezaji na usimamizi wa sheria zenyewe. Serikali hii na awamu nyingi zilizopita tatizo la muhali limetu haribia kupita kiasi, sheria zetu nyingi ni povu la soda.

Ilikuwa sheria hapa ya watu kuva *helmet* haya tembea wewe barabarani, wanaokamatwa ni watu ambao hawana bahati. Askari anaona leo nimeamka vibaya simama mbona huna *helmet* wameshapita pengine watatu rafiki zake, aah hivi, hivi, hivi anajidai kuandika na wewe unaona aah nikipelekwa Mahakamani itakuwa ngumu kumbe anaandika vile nyuma ya pazia, akishapewa chake haya piteni, tena piteni sio kwamba mteremshe haya nendeni. Kwa hivyo, yeze mwenyewe ile sheria baada ya kuisimamia anaimarisha ivunjwe.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu inaendeshwa kienyeji mno kiasi ambacho sisi hatuamini kwamba sheria hii, mimi siamini kwamba kwa uzoefu wa miaka nenda miaka rudi watu ambapo wameshajichimbia mali walizochukua, udhalimu uliofanywa, hakuna anayeulizwa hasa kuya-*reverse* yale ukafukua makaburi kama alivyosema Mwenyekiti, kasema kwamba kungekuwa na *grace period* ili watu kujiweka sawa kuanzia sheria hii tutakapoipitisha mpaka Rais atakapoiweka saini. Yeye kasema ianze Julai, kwa sababu Julai sisi tukijaaliwa pengine atakayekuwa hai katika Baraza hili *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tuwe hai tutakuwa tumeshamaliza masuala ya kuja humu tena, kila mtu na mbio zake huko anatafuta jimbo.

Kwa hivyo, kipindi hiki labda kiwasaidie wale ambao wanataka kujirekebisha. Mhe. Makame Mshimba unasema hapana tukiipitisha leo basi kesho Rais aweke saini. Mimi sheria hii naona tufanye tu kama wajibu wetu, lakini kama tunashindwa kutekeleza sheria rahisi ya *helmet*, tulipitisha sheria hapa sisi nakumbuka wakati Mhe. Machano ni waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mawasiliano Ikulu, magari ya abiria yawe na magurudumu mawili mawili nyuma na mbele, haya nenda weye leo. Watu wanakamatwa siku za mwanzo pale utafikiri maana yake, nenda leo hayo magari yatazame.

Kwa hivyo, nasema kama Baraza la Wawakilishi tunajiona wanyonge sana wengine, na mimi Mhe. Mwenyekiti, saa nyengine nitaona ah kweli ni wajibu wangu kutunga sheria, lakini kwa nini ni *waste time*, kwa nini nipoteze nguvu na jasho kusoma miswada, kusema mpaka maana yake unatoka kipovu hatimae utekelezaji na usimamizi wa sheria wenyewe haupo.

Kwa hivyo, tunafanya tu kama wajibu, sasa sheria ya *helmet*, ya magari ambayo ni usalama wa watu sasa hivi kama hazipo tena kama vile zile sheria zimefutwa. Hivyo kweli utakuja kutunza sheria hii mtu ana maghorofa, ana majumba, ana madubwesha gani, ana magari, wengine wana mameli mtu kaanza kazi hana hata kibanda, analala kwa mkwewe, analala kwao.

Mwaka mmoja utajiri alionao haumithiliki, ukisema hivyo mtu anakwambia ah hiyo ni hasadi, na iwe hasadi kwani mali yake, si yetu sisi tuiseme, lazima tuseme. Na hao viongozi wa umma nasema tena wengi sitaki kutaja hapa, kwa miaka mingi wamejizoesha katika hilo na hawa ndio watekelezaji wa sheria hii.

Kwa hivyo, mimi sidhani tufanyeni wajibu wetu najua hata kama niseme isipite hapa kwa sababu imeletwa na serikali itapita, lakini natahadharisha hilo, kwamba inafika mahali kwa sababu serikali zile sheria zenyewe hawazisimamii inakuwa ni kazi ya zeze.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saleh Nassor amesema hapa suala la undumilakuwili (*double standards*) ukishakuwa na *double standards* wewe ni kinyonga ukiingia kwenye *green*, ukiingia kwenye majani ya kavu una jani ya rangi kavu, hujulikani hasa rangi yako ni ipi.

Mheshimiwa hakuna jambo ambalo sisi wengine linatukera kwamba mkubwa anatoa amri tena hadharani kwa wadogo wake, lakini akishaondoka wale wadogo wake hawatekelezi amri, na ukiwashika sana wanakwambia ah bwana nyinyi mbona mnatuhangaisha. Kweli tumeambiwa vile pale, lakini tumeitwa tukaambiwa bwana yale yalikuwa maneno ya kisiasa tu.

Mhe. Subeit amesema tumeondoka hapa tena Baraza hili Waheshimiwa ikaazimia kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulika na mambo ya vitambulisho vya *Zan ID*, kaka yangu, rafiki yangu, jirani yangu Dkt. Mwinyihaji amechukua juhudu tumekwenda Pemba kila Wilaya amewaita masheha wote, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, watu wa vitambulisho zikapigwa hotuba pale mpaka Dkt. Mwinyi akala jasho.

Mkurugenzi wa Vitambulisho akasema mpaka akadata, anatokea Sheha anasema sisi hatuwezi kufanya hivyo bwana, anasema mbele ya waziri hivyo, hivi hivi kavu kavu. Na kweli bwana walikithiri yule sheha mwisho alipandishwa cheo ndio maadili hayo, hayo ndio maadili, Sheha wa Mtambile, hayo ndio maadili. Sasa hii ni *double standards*, mnazungumza *very serious* maamuzi ya Baraza kwamba nendeni mkafanye hili, mkafanye hili, Sheha ana ubavu gani wa kuvunja amri ya Waziri.

Mimi nambieni halafu akanyamaziwa kimya maana yake ni kwamba huyo waziri mwenyewe kasema pale kuondoa wadudu mkizini, lakini utekelezaji ni ule ambao unatufanya, sikuja navyo hapa. Mimi nina vyeti vitavyotakiwa vya kuzaliwa 208 nimewaambia watu wangu kama Mwakilishi amekuja kanilalamikia nikawaambieni nataka ushahidi, wametoo *photocopy* ninazo *photocopy* 208 vyeti halisi masheha wanawaambia nani, hatutoi fomu nendeni mnakotaka kwenda, maana yake nini?

Na sheha sheria ile inasema hatakiwi kumuomba mtu fomu, kumtaka mtu cheti cha kuzaliwa si kazi yake, ye ye ni kuthhibitisha, ye ye anakaa katika shehia yake ametimiza miaka mitatu mpe fomu. Leo sheha anakwambia kama hukunionesa cheti cha kuzaliwa sikupi fomu, cheti cha kuzaliwa anapewa anasema sikupi fomu, na wengine huyo ambaye atakayebahatika wanatolesha watu shilingi elfu tano mpaka elfu kumi na mbili, masikini ya Mungu halafu unasema tuna sera ya kupunguza umasikini. Masikini ya Mungu fomu ambayo imeandikwa pale shilingi mia tano unamtolesha mtu shilingi elfu kumi na mbili, unaichukua fomu unahangaika mnakwenda kupigwa picha miezi tisa hupei kitambulisho, lakini mwengine mnakwenda kupiga picha wiki tatu keshapewa, *sub standards*. Hapa sheria hii nakwambieni tena kuna watu mtawaonea, na kuna watu mtawapendelea, hakuna uadilifu, uadilifu uko wapi.

Kwa hivyo, mimi nazungumza kwa mantiki kwamba tusifanye jambo kwa sababu ya kufanya tu, kama tutafanya jambo watu waonekane kwamba hili jambo limefanywa, watu wamelipwa na linatekelezwa na serikali. Hata serikali ukitaka kuihoji, Baraza hili likitaka kuhoji basi unatiwa mnyororo, *very live, example* nitakupeni.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mujibu wa kanuni ya Baraza hili nimepeleka hoja binafsi nikamu-*offer* Spika, tena sababu za msingi kabisa. Hoja yenyewe kuhusiana na kutaka serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, hoja binafsi.

Kwa mujibu wa kanuni zote sikusahau kanuni hata moja tangu Ijumaa nime-*submit* na barua nasikia maneno ya njiani tu kwamba ile mpaka mwezi wa Machi, *is useless*. Hoja hii binafsi Waheshimiwa ni ya kujadiliwa kipindi hiki ndio kazi zetu sisi hapa tumekuja kuwakilisha watu kutafuta haki zao, kuihoji serikali, sasa hii si *double standardness*, tena pengine *one hour* tu ingetosha.

Hata ukisema kwamba niwasilishe mwezi wa Machi, Aprili watu wanapiga kura ya maoni nafikiri ni CCM peke yao watapiga ndio, UKAWA hatupigi tunakuachieni uhuru mjifarague atakayepiga kura nne nne haya twendeni, lakini yejote anayetaka kupiga kura awe na kitambulisho cha Mzanzibari. Tumeambiwa na Mkurugenzi wa Vitambulisho kama utapigwa picha leo si zaidi ya wiki mbili watu wana miezi 10 hawajapewa *Zan ID*, ukienda sababu unaambiwa maana yake *material* iliyoletwa sijui ni *inferior* sijui ni *fake*, maneno hayo unanambia mimi, *material* lakini wengine wanapewa maana kuna *material* namna mbili basi; za watu wengine ni *fake* na watu wengine nzuri, wapi na wapi.

Nimeoneshwa kitambulisho kime-*expire* mwaka 2010, lakini alichopewa kapewa mwaka 2013 kina *expire* Januari, 2015. Haya umeona wapi kitambulisho namna hiyo, maana vitambulisho vyote kama ni miaka mitano au kumi, maana yake hakifiki hata miaka miwili, mwaka 2013 mpaka 2015 Januari kisha-*expire* ajabu, unakwenda na cheti za kuzaliwa unakipata kwa sheria zote na taratibu unakwenda mtu anakwambia hiki *fake*, kakiona tu, hiki *fake*. Jamani mbona mnaingiza watu katika umasikini, hivyo mambo haya ni mpaka lini?

Mhe. Mwenyekiti, najua kuna wachangiaji wengine, kwa hivyo hoja hii binafsi narudia tena mtu anapoikataa kwa sababu zote zile mimi nasema ni njama tu, *sub standards*. Mara nydingi hapa hoja binafsi ni adimu.

Hoja ya Mhe. Hamza ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi bana bana wee sijui angalau mimi nimeambiwa, siaambiwa rasmi nasema, lakini mpaka hii leo Baraza tuna kesho na keshokutwa tu na Mswada huu ni mkubwa. Bado na-*appeal* kwamba kama Mhe. Spika, alikuwa na dhamira hiyo namuomba sana kwa maslahi na manufaa ya Wazanzibari tena wote, kuna watu mimi jimbo langu pekee watu 400 wana stakabadhi ya kupata *Zan ID*, wengine wamekwenda Wete mara tano, kwenda Wete na kurudi kutoka Ole ni shilingi 2500, mtu amekwenda mara nne shilingi 10,000 masikini ya Mungu hajapewa, wapi na wapi. Mwisho wanasema sendi na hiyo ndio dhamira, ukienda mara mbili hujapata unasema aah, bwana ee kwani lipi, mkakati.

Mhe. Mwenyekiti, amekuja kijana kunilalamikia amepoteza, kupoteza ni jambo la kawaida, kitambulisho za kupigia kura kenda kwa Sheha apate barua ndiyo taratibu ili aende polisi na polisi wampe barua aende Tume ya Uchaguzi, kamwambia sikupi kwa nini upoteze, *last minute* ilipoingia kakara kakara amemtoza shilingi 10,000 ndio, shilingi 10,000 ndio kampa barua aende polisi. Mawaziri wapo hapa wanaoshughulika na hayo.

Sasa unapoyaachia haya maana yake ni wewe mwenyewe unashajihisha, ndio nikakwambia kwamba maadili ya viongozi jamani ni mapana, unapomuachia mtu anaharibu na wewe una uwezo wa kumuondoa, haya nazungumza huyu Sheha atatafutwa na tuko hapa hapa ataongezwa cheo, huyu kama Sheha wana ukoplo au usajenti. Lakini wangkuwa wana vyeo hivi nakwambai huyu angeambiwa heko, ongeza cheo hapo kuwa mkuu wa masheha.

Mawaziri mnatu-*disappoint*, tunafika mahali tunasema kwamba haya mnafanya kwa makusudi, kama mlikuwa hamuyajui sasa mnayajua, huwezi kunambia mimi sijui, nishakwambia sasa njoo unambie ni nani, sitaji hapa, nitakwambia ni fulani, aliyetoleshwa shilingi 10,000 fulani, na ushahidi nimemchukua mimi mwenyewe kwenda polisi kijana huyo, keshahangaika mara nne kwenda kwa Sheha. Sasa jamani wapi na wapi.

Mhe. Mwenyekiti, najua unataka kunambia basi. Juzi nilikuwa naangalia *Citizen TV* ya Kenya, wanafunzi wa skuli fulani nimeisahau unajua majina ya Kenya ni madogo lakini magumu, waliandamana kudai eneo lao lililovamiwa na wananchi, eneo la skuli. Askari polisi wakaenda kule na zogo lao, balaa, mabunduki wakapiga mabuti, almuradi wanafunzi wakaathirika, mabomu ya machozi maandamano ya wanafunzi hawana chochote hata penseli, sio kwamba wamechukua labda marungu. Wanafunzi *innocently*, kuonesha tu, *ku-protect* kwamba eneo letu la skuli jamani limechukuliwa. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, askari wale namalizia.

**Mhe. Mwenyekiti:** Muda wako umekwisha.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Nakushukuru Mwenyekiti.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kwanza nikuombe kwamba muda wangu ulionipa sasa hivi mpaka saa mbili kasorobo kwa kweli utakuwa haunitoshi sana. Kwa hivyo nitoe tahadhari na nikuombe kwa heshima zote hasa kwa vile ni mwanamke, ni mlezi, kesho unipatie muda wangu niendelee tena.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kuchangia mswada huu kwa kuipongeza serikali, nilitamani ndani ya muda wangu wa uongozi mswada huu uje nikiwa Mwakilishi. Kwa hivyo, kama serikali wamefanya haki kwa mtazamo wangu basi wamefanya haki kwa kuleta mswada huu kipindi hiki, ingawa wamechelewa kwa sababu nchi imeangamia sana, lakini *chelewa usike* na sasa tufanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri ametoa tafsiri kwenye mswada huu kuhusu maana ya maadili, amesema kwamba maadili maana yake ni maadili ya viongozi wa umma kama ilivyoleezwa katika sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi si mtaalamu wa lugha lakini nataka niwaambie wenzangu na Wazanzibari wote kwa jumla, kwa mtu wa kawaida Mhe. Mwenyekiti ukimwambia neno 'maadili' maana yake ni adabu. Maadili maana yake ni adabu, maadili maana yake ni heshima, maadili maana yake ni nidhamu, maadili maana yake ni uadilifu, maadili maana yake ni utaratibu wa sheria, maadili maana yake ni uwajibikaji.

Mhe. Mwenyekiti, yanapoondoka yote hayo kiongozi huyo huwa hana maadili, awe na adabu, heshima, uadilifu, nidhamu, utaratibu wa sheria na uwajibikaji uliopaswa na sheria. Haya yakikamilika kiongozi huyu kwa namna yoyote ile huambiwa kiongozi huyu ana maadili na yakiondoka hata kama mtu atampamba, mpambe utakavyo lakini madhali yameondoka haya kiongozi huyu huwa hana maadili, ni sawa sawa na kusema kwamba mtu yule ana mguu mzito kumbe umekusudia kusema kwamba mtu huyu ana tende.

Kwa hiyo, maadili ni neno la Kiswahili ambalo limeficha mambo lakini ukilichambua unaweza ukapata maneno mengi ambayo kwa kweli ndiyo hasa yanatakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mswada huu binafsi niseme kwamba nawapongeza na nawaunga mkono kwa asilimia mia moja. Niseme kwamba kwa sababu zozote zile ambazo mswada huu mtu ataukataa kwa mtazamo wangu Mwenyekiti kama si hofu ile ya utekelezaji basi ni dhahiri kwamba anakusudia kujificha kwenye suala hili la maadili, lakini kama kweli kiongozi anakusudia kuwajibika na kuwafanya vyema Wazanzibari ni lazima Mswada huu auunge mkono na aharakishe utiwe saini ili nchi isiendelee kuangamizwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 55 kuna tafsiri ya neno la ulevi wa kupindukia, maana yake ni ulevi wa kupita kiasi hadharani ambapo mtu atashindwa kufahamu anachokifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napendekeza kwamba usiwe ulevi wa kupindukia bado ule ni ulevi tu, ulevi ni ulevi tu uwe wa kuonja, iwe wa madaraka, iwe wa chochote, kwa sababu tuisubiri mpaka mtu apindukie. Mwenyekiti wengine huehezea chupa 20 humu hawajalewa na wengine mbili tu wanaanguka, wengine maneno tu hulewa. Kwa hivyo, ulevi uwe ulevi tu, iwe wa kupindukia, iwe wa kuonja, iwe mdogo au mkubwa ulevi ni ulevi tu.

Mhe. Mwenyekiti, kiongozi ambaye analewa hadharani watu wanamuona hata kama hakuanguka, hata kama hakupinduka huyu hafai kuwa kiongozi kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka nilichangie kwenye ukurasa wa 56 kifungu cha 7(3)(b). Hapa imetangazwa kwamba mtu ambaye hafai kuwa mwenyekiti ni mtu ambaye ametangazwa kafilisika. Kafilisika ni neno pana sana inawezekana kisiasa, inawezekana kimali, ningombaa Mwanasheria au Waziri wetu basi atuwekee sawa neno hili ili asijekuwa mmoja amefilisika kisiasa akaambibiwa hafai mwengine akawa badala ya kupata chejio sasa anauza bofulo akaambibiwa huyu anafaa. Kwa hiyo, naomba hili neno "kafilisika" liwekwe sawa ili kila mtu sheria hii aelewewe kwa lugha nyepesi sana.

Kifungu chengne ni kifungu cha 16(1)(g). Kifungu hiki nakipongeza kwamba mtu ambaye atalazimika kutangaza mali au kutangazwa hadharani ni yule mtu ambaye mali zisizohamishika ambazo zinamilikiwa kwa njia ya faida na ambazo zinajiedhesa kwa njia ya wakala.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme wazi kabisa kwamba nimekuja na orodha, orodha hii ina viongozi wa kisiasa 17, wote wamechukua ardhi ndani ya Jimbo la Kiwani ninao hapa. Kabla ya Rais kutoa tangazo saini hii naomba ardhi ile irejeshwe haraka, haiwezekani mtu mmoja kumiliki *square meter* 4,400 haiwezekani; wengine ni Mawaziri, si wangu huu sikuutoa Mwambe mimi huu nimetumia haki yangu ya kanuni nimeomba serikalini nimepewa. Haiwezekani mtu wa kawaida kumiliki *square meter* 4,400 rejesheni serikalini, rejesheni kwako kwa wananchi. Naomba nimitaje mmoja ili iwe mfano, wengine nataka niwafiche ili mnitafute niseme huu ndio ule utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, mmoja anaitwa Zainab Khamis Shomari ana *square meter* 3,751 za ardhi ya Mwambe haiwezekani, rejesheni haraka serikalini mali ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, watu hao 17 nitakupatia *copy* uwaombe mali ya serikali irejeshwe haraka serikalini, msiyatangazie watu kwamba nchi hii ina utawala bora, nchi hii ina heshima kumbe wengine wanajikumbizia mali baadaye siku ya uchaguzi mnawaambia kwamba chagueni bwana maisha bora, maisha bora unayaleta hapa mpaka mbinguni? Kwa hivyo naomba sana kwa heshima zote kabla ya kutiwa saini sheria hii mali za serikali zirejeshwe serikalini kwa utaratibu wa kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo na mimi nimuombe sana Mhe. Rais na niungane mkono na Mhe. Makame Mshimba tuwapatie viongozi wetu wa serikali miezi sita kama ni *grace period*, warejeshe mali zao serikalini haraka. Baada ya hapo mali yoyote ya serikali ambayo imechukuliwa kinyume na sheria irejeshwe haraka, hatuwezi kuwa watumwa wa watu wetu, watu wamechukua mali za serikali muda mrefu na wanalindwa na wanajulikana. Kwa hivyo, mswada huu ndio jibu la wanyonge wa Zanzibar.

Nataka nimwambie Mhe. Waziri, hii ni sheria na amuombe Mhe. Rais atie saini haraka, vyenginevyo ikifika miezi sita nchi inamalizwa. Yuko mtu mmoja alitujia hapa akatwambia kwamba kuna mtu fulani ana *account* nje ya nchi, watu wana mali nje ya nchi mswada huu ndio suluhisho la watu hao, lazima kila mtu atangaze mali na niombe asichaguliwe mtu kuwa Mbunge, Mwakilishi au Rais kama hajatangaza mali yake kwanza.

Mwakilishi au Rais kama hajatangaza mali yake kwanza na sio atangaze tu, apimwe, je, mimi Hija Mwakilishi miaka 10. Je, mshahara wake una uwezo wa kumiliki ghorofa 10? Lazima tupimwe, ni kwa nini mtu huyu amekaa miaka 5 lakini ana maghorofa zaidi ya 7. Huo ndio wajibu wa serikali na huo ndio wajibu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwatoe hofu wenzangu ukiwa unaogopa kuchunguzwa wewe itakuwa na wewe una tatizo vile vile; ikiwa kuna kiongozi anaogopa kuchunguzwa nalo ni tatizo, kila mtu apekuliwe mpaka nywele na tuambiwe nani mali hii ni yake au mali hii ni ya hadaa na kama ni ya hadaa arejeshe, sio afungwe, kufungwa haitusaidii sisi, kufungwa haisaidii, arejeshe serikalini halafu ikibidi kufungwa na afungwe. Lakini kwanza serikalini irejeshwe mali ile ili wananchi wafaidike halafu hatua nyengine zichukuliwe, lakini masuala ya muhali kwamba maana yake viongozi wakubwa wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mmoja, nilipokuwa nafanya utafiti wa sheria hii nilikwenda kwa kiongozi mmoja mstaa fuwa Serikali hii ya Zanzibar, ameshika uwaziri katika awamu tano na wizara tofauti akanambia siku hiyo nilisikitika na bado yuko hai. Leo simtaji kwa sababu mumemgaia bodi musije mukamnyang'anya. Alinambia waziri fulani niliombwa na Marehemu Dr. Omar Ali Juma nikamtafute nilipokwenda anapiga matofali Mbweni, leo ana maghorofa kumi mimi sina. Ananambia zaidi ya nyumba hii ya Jeshi niliyogaiwa sina nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, hao ndio viongozi waadilifu, akanambia kwa mdomo wake naomba nimnukuu Mhe. Mwenyekiti, kwamba "nchi hii watu ambaa ni waaminifu ni Dr. Ali Mohammed Shein, mimi na Mhe. Seif Sharif Hamad". Siwezi kumshawishi, ananambia nchi hii ambaye hana mali ya umma ni Dr. Ali Mohammed Shein mimi na Seif Sharif Hamad waliobakia wengi mtihani, lazima watu wachunguzwe, na Abubakar Khamis Bakary ee, sawa. Wengine wachunguzwe mali ambayo imepatikana kwa njia ya hadaa lazima irejeshwe serikalini, lazima, lazima.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani mtu anaiba ndizi na doriani afungwe lakini mtu aliyechukua mali za umma mseme mnaogopa maana ni viongozi wakubwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hija Hassan Hija malizia.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, sio nimalizie nadhani uniwekee *comma*, nina mambo mazito ya kesho tukijaaliwa sjafika hata robo Mhe. Mwenyekiti, nakuhestimu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sawa utakuwa ni mchangiaji wa mwanzo.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofî*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana, nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati na niwashukuru wachangiaji wote ambao leo wameweza kuchangia na wengine ambao walikuwa wasikilizaji niwashukuru kwa utulivu wao. Kabla ya kuakhirisha kikao naomba kusoma matangazo mawili muhimu.

Tangazo la kwanza Wajumbe wote wanaarifiwa kuwa kesho Alkhamisi tarehe 29/01/2015 kutakuwa na hafla ya ufunguzi wa msikiti wa Baraza la Wawakilishi itakayofanyika wakati wa adhuhuri ambapo swala ya adhuhuri itasaliwa kwa pamoja.

Kwa taarifa hii, kikao kitaakhirishwa saa 6:40 za mchana kwa ajili ya kuwapa Wajumbe nafasi ya kushiriki katika swala ya ufunguzi huo. Mgeni rasmi wa hafla hiyo atakuwa ni Mufti Mkuu wa Zanzibar na wageni wengine waalikwa watakuwa ni Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar, Katibu Mtendaji Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Mashekhe na Waislamu wengineo. Sote tunaombwa kuhudhuria na baada ya hafla hiyo kutakuwa na chakula cha pamoja.

Tangazo la pili, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza wanaarifiwa kuwa kesho saa nane na nusu mchana baada ya kumalizika kwa hafla ya ufunguzi wa msikiti wetu kutakuwa na ile safari yetu ya kuonana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa Wajumbe mpaka kufikia hapa leo tunaakhirisha kikao chetu hadi kesho tarehe 29/01/2015 saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1:46 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 29/01/2015 Saa 3:00 asubuhi)*